# Wanawake katika Uislamu

**Ukilinganisha na Wanawake katika**

**Mafundisho ya Kiyahudi-Kikristo:**

**Hadithi za kubuni na uhakika**

DR. SHERIF ABDEL AZIM

Ph.D. - QUEENS UNIVERSITY,

KINGSTON, ONTARIO, CANADA

# Yaliyomo

*UTANGULIZI* ______ *3*

*SEHEMU 1- KOSA LA HAWA (EVA)* ______ *8*

*SEHEMU 2- URITHI WA HAWA* ______ *11*

*SEHEMU 3 - MABINTI WANAOTIA AIBU* ______ *19*

*SEHEMU 4 – ELIMU KWA WANAWAKE* ______ *22*

*SEHEMU 5 – MWANAMKE MWENYE HEDHI SI MSAFI* ______ *25*

*SEHEMU 6 – HAKI YA KUTOA USHAHIDI* ______ *28*

*SEHEMU 7 - UASHERATI* ______ *32*

*SEHEMU 8 - KULA KIAPO NA KUWEKA NADHIRI* ______ *35*

*SEHEMU 9 – MALI ZA MKE* ______ *39*

*SEHEMU 10 – TALAKA* ______ *46*

*SEHEMU 11 – AKINA MAMA* ______ *60*

*SEHEMU 12 – MIRATHI KWA WANAWAKE.* ______ *65*

*SEHEMU 13 – HALI MBAYA YA WAJANE* ______ *69*

*SEHEMU 14 – UKEWENZA* ______ *73*

*SEHEMU 15 – HIJABU* ______ *87*

*SEHEMU 16 – HITIMISHO* ______ *97*

# UTANGULIZI

Miaka mitano iliyopita, nilisoma makala katika gazeti la Toronto Star toleo la Julai 3, 1990, yenye kichwa ‘‘Uislamu sio pekee wenye itikadi ya kuwatukuza wanaume’’, iliyoandikwa na Gwynne Dyer. Makala hiyo ilichambua majibu makali mno kutoka kwa washiriki wa mkutano juu ya wanawake na kushika Madaraka uliofanyika Montreal ili kujibu maelezo ya mtetezi maarufu wa haki za wanawake kutoka Misri, Dr. Nawal Saadawi. Taarifa yake ambayo kisiasa si sahihi inajumuisha: ‘‘*viini vyenye vikwazo vingi kwa wanawake vinapatikana, kwanza kabisa katika Uyahudi katika Agano la Kale, kisha katika Ukristo na katika Quran’’ ‘‘dini zote zinatukuza wanaume kwa sababu zote zimeanzishwa kutokana na misingi ya jamii zenye kutukuza wanume*’’ na ‘‘*hijabu za wanawake si matendo ya Kiislamu peke yake lakini ni utamaduni wa kale uliorithiwa wenye kufanana na dini ya kisista (utawa).*’’ Washiriki walishindwa kuvumilia na kukaa chini, huku imani zao zikilinganishwa na Uislamu. Kwa hiyo, Dr. Saadawi alipokea mlolongo wa kukosolewa. ‘‘*Maelezo ya Dr. Saadawi hayakubaliki. Majibu yake yanaonyesha ukosefu wake wa kutofahamu imani za watu wengine,’’* alitamka Bernice Dubois wa Maendeleo ya Kinamama Duniani. *‘‘Lazima nizuie’’* alisema mwanajopo Alice Shalvi wa mtandao wa wanawake wa Kiisraeli, ‘‘*Hakuna itikadi ya hijabu katika Uyahudi.*’’ Makala hiyo

imetoa upinzani huo mkali kwa mtazamo mkali wa Kimagharibi, kwani kuusingizia Uislamu kuwa ndio unaotekeleza hayo ni sehemu ya urithi wa utamaduni wa Kimagharibi. *''Watetezi wa haki za Wanawake wa Kikristo na Kiyahudi hawakuridhia kuendelea kukaa na kujadili kwa namna ile ya kuwapo kundi moja na Waislamu, ambao ni Waovu.''* Imeandikwa na Gwynne Dyer.

Sikushangazwa kuona washiriki wa mkutano huo wameshikilia msimamo mbaya dhidi ya Uislamu, na hasa hasa inapohusika kadhia ya wanawake. Katika nchi za Magharibi, inaaminika kuwa Uislamu ndio alama ya kuwadhalilisha na kuwadunisha wanawake kupita kiasi. Ili kufahamu kwa kiasi gani imani hiyo ilivyo, inatosha kuonyesha kuwa Waziri wa Elimu wa Ufaransa, nchi ya mabadiliko (Voltaire), hivi karibuni ameagiza wafukuzwe wasichana wote wa Kiislamu wanaovaa hijabu watolewe shule za Ufaransa![1] Mwanafunzi msichana wa Kiislamu avaae kitambaa cha kufunika kichwa ananyimwa haki yake ya kupata elimu nchini Ufaransa huku wanafunzi wa Kikatoliki wavaao misalaba au wanafunzi wa Kiyahudi wavaao kikofia cha Kiyahudi hawazuiwi. Mandhari ya Polisi wa Kifaransa wakiwazuia wasichana wa Kiislamu wanaovaa vitambaa vya kufunika vichwa wasiingie shule zao za sekondari ni jambo lisilosahaulika. Jambo hilo linaibua kumbukumbu ya tukio lingine la fedheha linalomuhusu

[1] The Globe and Mail, Oct. 4, 1994.

Gavana George Wallace wa Alabama mwaka 1962 akiwa amesimama mbele ya geti la shule huku akijaribu kuzuia kuingia wanafunzi weusi ili kuulinda Ubaguzi wa Rangi wa shule za Alabama. Tofauti ya matukio mawili hayo ni kuwa wanafunzi weusi walionewa huruma na watu wengi wa Marekani na dunia nzima.

Rais Kennedy alitumia jeshi la ulinzi wa taifa la Marekani ili kulazimisha kuingia kwa wanafunzi hao weusi. Kwa upande mwingine, wasichana wa Kiislamu, hawakupokea msaada wowote kutoka kwa yoyote yule. Sababu yao ilikuwa inatia huruma kidogo sana ndani ya Ufaransa au nje. Sababu yenyewe ni yenye kuenea sana nayo ni kutofahamika vizuri na woga juu ya kila kitu cha Kiislamu ulimwenguni leo hii.

Kile kilichonivutia sana katika mkutano wa Montreal kilikuwa ni swali mojawapo: Je, maelezo yaliotolewa na Saadawi, au yoyote katika wakosoaji wake ni ya uhakika? Kwa maneno mengine, Je, dini ya Uyahudi, Ukristo na Uislamu zina itikadi inayofanana juu ya wanawake? Je, dini hizi zinatofautiana kiitikadi? Je, ni kweli kuwa, Uyahudi na Ukristo unawatendea vyema wanawake kuliko Uislamu? Ukweli ni upi?

Si rahisi kutafuta na kupata majibu ya maswali haya magumu. Ugumu wa kwanza kabisa ni kuwa mtu anatakiwa awe mwadilifu na asiegemee upande wowote au, kwa uchache, afanye kila liwezekanalo ili awe hivyo. Na hivyo ndivyo unavyofundisha Uislamu. Quran imewafundisha

*Waislamu* waseme ukweli hata ikiwa dhidi ya watu wa karibu yao. *''...Na sema (katika shahada na penginepo) Semeni kwa insafu ingawa ni jamaa;* Quran (6: 152) *''Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowapo ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu, au (juu ya) wazazi (wenu) na jamaa (zenu). Akiwa tajiri au masikini (wewe usitazame).* (Quran 4: 135).

Jambo jengine lilogumu sana ni kuushinda upeo wa mapokezi na kuvumilia kadhia hiyo. Kwa hiyo katika kipindi cha miaka michache ya hivi karibuni, nimetumia masaa mengi kuisoma *Biblia, ensaiklopidia ya dini na ensaiklopidia ya Uyahudi* nikitafuta majibu. Pia nimesoma vitabu vingi vinavyojadili nafasi ya mwanamke katika dini mbalimbali vilivyoandikwa na wanazuoni (wataalamu), watetezi, na wakosoaji. Taarifa zilizowasilishwa katika sura zifuatazo zinaleta matokeo muhimu yaliyopatikana kutokana na uchunguzi huu wa kinyenyekevu. Sidai kuwa sikuegemea upande wowote ule kikamilifu. Kwani jambo hilo lipo nje ya uwezo wangu. Kile ninachoweza kusema ni kuwa nimejaribu, kwa kupitia utafiti huu, nikaribie ukamilifu wa Quran *wa kuongea kiadilifu*.

Ningependa kusisitiza katika utangulizi huu kuwa lengo langu katika utafiti huu si kuupaka matope Uyahudi wala Ukristo.

Tukiwa kama Waislamu, tunaamini kuwa kuna asili ya utakatifu kwa mitume wote wawili. Hakuna mtu atakaye

kuwa Mwislamu wa kweli bila ya kuwaamini Musa na Yesu kwamba wao ni mitume mikuu ya Mwenyezi Mungu. Lengo langu ni kuuthibitisha na kuutukuza Uislamu, na kuupa ujumbe wa mwisho wenye kuaminika, utokao kwa Mwenyezi Mungu kwenda kwa jamii ya wanadamu kile inachokistahiki kwa muda mrefu katika nchi za Magharibi. Vile vile napendelea kutilia mkazo kuwa mimi nazingatia na najihusisha sana na mafundisho ya dini husika. Na hilo, ndilo nitakalojihusisha nalo, kwa kiasi kikubwa, nafasi ya mwanamke katika dini tatu kama ilivyo katika vyanzo asilia vya dini hizo na sio mambo yanayotendwa na mamilioni ya wafuasi wa dini hizo ulimwenguni leo hii.

Kwa hiyo, ushahidi mwingi utakaokuwepo katika kitabu hiki umetokana na Quran, hadithi za mtume Muhammad (S.A.W.), Biblia, Talmudi (kitabu cha Wayahudi), na maneno ya baadhi ya Mapadri wa makanisa wenye mvuto mkubwa na ambao mitazamo yao imetoa mchango usiokadirika katika kuufahamisha na kuutengeneza Ukristo. Hamu hii ya kupata vyanzo asilia inafungamana na ukweli kwamba kuifahamu dini fulani kutokana na mitazamo na mienendo ya baadhi ya wafuasi wake kwa majina ni upotoshaji. Watu wengi wanachanganya utamaduni na dini, na wengine wengi hawajui vitabu vyao vya kidini vinasema nini, na wengine wengi hawajali kabisa.

# SEHEMU 1

# KOSA LA HAWA (EVA)

Dini tatu hizi zinakubaliana juu ya hakika moja ya msingi: wanawake na wanaume wote wameumbwa na Mungu, ambaye ni Muumba wa ulimwengu wote. Hata hivyo, tofauti zinaanzia punde tu baada ya kuumbwa mwanamume wa kwanza - Adam na mwanamke wa kwanza – Hawa. Itikadi ya uumbwaji wa Adam na Hawa kwa Wayahudi na Wakristo imesimuliwa, kwa ukamilifu, katika kitabu cha mwanzo 2:4-3:24. Mungu aliwakataza wote wawili wasile matunda ya mti uliokatazwa. Nyoka alimshawishi Hawa ale matunda ya mti huo na Hawa, naye, akamshawishi Adam ale pamoja naye.

Wakati Mungu alipomkaripia Adam kwa alichokifanya, Adam naye akamtupia Hawa lawama zote, Mwanzo 3:12 *‘‘Adam akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala.’’ Kwa matokeo hayo, Mungu alimwambia Hawa: Mwanzo 3:16 “Akamwambia mwanamke, Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala.’’ Na kwa Adam Mungu alimwambia: ‘‘Kwa kuwa umesikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti… ardhi imelaaniwa kwa ajili*

*yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako…''* Itikadi ya Kiislamu juu ya uumbwaji wa mwanzo inapatikana sehemu nyingi ndani ya Quran, kwa mfano:

*''(Kisha Mwenyezi Mungu akasema kumwambia Nabii Adam) ''Na wewe Adam! Kaa Peponi pamoja na mkeo, na kuleni mnapopenda, lakini msiukaribie mti huu msije kuwa miongoni mwa waliodhulumu (nafsi zao.) Basi Shetani (naye ni yule Iblisi), aliwatia wasiwasi ili kuwadhihirihishia aibu zao walizofichiwa, na akasema: ''Mola wenu hakukukatazeni mti huu ila (kwa sababu hii:) msije kuwa Malaika au kuwa miongoni mwa wakaao milele (wasife).'' Naye akawaapia (kuwaambia): ''Kwa yakini mimi ni mmoja wa watowaoshauri njema kwenu'' Basi akawateka (wote wawili) kwa khadaa (yake). Na walipouonja mti ule aibu zao ziliwadhihirikia na wakaingia kujibandika majani ya (miti ya huko) Peponi. Na Mola wao akawaita (Akawaambia): ''Je, sikukukatazeni mti huu na kukwambieni ya kwamba Shetani ni adui yenu aliyedhahiri?'' Wakasema: "Mola wetu! Tumedhulumu nafsi zetu; na kama hutatusamehe na kuturehemu, bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa wenye khasara (kubwa kabisa)''* (Quran 7:19-23).

Mtazamo yakinifu juu ya fikra mbili hizi kuhusu kisa cha Uumbwaji, unafunua baadhi ya tofauti za kimsingi. Qurani, kinyume na Biblia, inatoa lawama zilizo sawa sawa kwa wote wawili Adam na Hawa kwa makosa yao. Hakuna sehemu hata moja katika Quran ambapo mtu atakuta hata kidokezo kidogo sana ambacho kinaashiria kuwa Hawa alimshawishi

Adam ale katika mti huo au hata kuwa Hawa ndiye aliyekula kwanza kabla ya Adam. Hawa katika Quran si mshawishi wala si mlaghai na si mdanganyifu. Zaidi ya hayo, Hawa si wa kulaumiwa kwa machungu ya uzazi. Mungu, kulingana na Quran, hamuadhibu yeyote kwa kosa la mwingine. Wote wawili, Adam na Hawa, wametenda dhambi kisha wakamuomba Mungu msamaha Naye akawasamehe wote wawili.

# SEHEMU 2

# URITHI WA HAWA

Taswira ya kuwa Hawa ni mshawishi iliyo ndani ya Biblia imeleta matokeo ya athari mbaya kwa kiasi kikubwa kwa wanawake katika mafundisho ya Uyahudi-Ukristo. Wanawake wote waliaminiwa kuwa wamerithi kutoka kwa mama yao, Hawa wa Kibiblia, mambo mawili: zambi zake na hila zake. Kwa hiyo, wanawake wote wakawa hawaaminiwi, madhaifu wa uadilifu, na waovu. Kupatwa na hedhi, mimba, na kuzaa; vitu hivi vilizingatiwa kuwa ni adhabu ya uadilifu kwa dhambi ya milele ya kulaaniwa kwa jinsi ya kike. Ili tufahamu vizuri ni naman gani mkanganyiko mbaya juu ya Hawa wa Kibiblia ulivyokuwa kwa vijukuu vyake vya kike vyote tunalazimika kutazama maandiko ya baadhi ya Wayahudi na Wakristo muhimu sana wa kila zama.

Hebu acha tuanzie na Agano la Kale na tuone dondoo kutoka katika kile kiitwacho *Maandiko ya Busara* ambayo kwayo tunakuta: *“Naona uchungu sana kuliko uchungu wa kifo mwanamke ambaye ni ghiliba, ambaye moyo wake ni mtego na mikono yake ni minyororo. Mwanamume anayempendeza Mungu atamuepuka mwanamke huyo, lakini muovu atatekwa na mwanamke huyo… Wakati nilipokuwa naendelea kutafuta bila kupata, nilipata mwanamume mmoja wa kuaminika*

*miongoni mwa maelfu, lakini sijapata hata mwanamke mmoja wa kuaminika miongoni mwa wanawake wote''*. (Ecclesiastes 7:26-28).

Katika sehemu nyingine ya maandiko ya Kiyahudi ambayo yanapatikana katika Biblia ya Kikatoliki tunasoma: *"Hakuna uovu unaotokea sehemu yeyote unaokaribiana na uovu wa mwanamke.... Dhambi huanza kwa mwanamke na tunamshukuru mwanamke kwa kuwa sote lazima tufe'';* (Ecclesiasticus 25:19-24).

Wataalamu wa dini ya Kiyahudi wameorodhesha laana tisa zinazowatesa wanawake ikiwa ni matokeo ya Kuporomoka: *"Yeye ametoa laana tisa na kifo kwa mwanamke: Mzigo wa damu ya hedhi na damu ya bikra; mzigo wa kubeba mimba; mzigo wa kuzaa; mzigo wa kulea watoto; kichwa chake kinafunikwa kama vile mtu yupo katika maombolezo; mwanamke anatoboa masikio yake kama vile mtumwa wa kudumu au mjakazi ambaye anamtumikia bwana wake; mwanamke asiaminiwe kuwa ni shahidi; na baada ya yote hayo… kifo.''*[2]

Kwa hivi sasa, Wayahudi wakiume wa Kiorthodoksi katika sala zao za kila siku asubuhi wanakariri *"Baraka ni za Mungu mfalme wa ulimwengu wote kwa kuwa hajaniumba mwanamke";* Wanawake, kwa upande mwingine, wanakariri

---

[2]Leonard J. Swidler, Women in Judaism: the Status of Women in Formative Judaism (Metuchen, N,J: Scarecrow Press, 1976) p. 115.

"*shukraniii ni za Mungu kila asubuhi kwa kuniumba kulingana na Matakwa yake.*"[3]

Dua nyingine inayopatikana katika vitabu vingi vya dua za Kiyahudi: "Shukrani ni za Mungu kwa kuwa hajaniumba nikiwa mtu wa mataifa (mtu ambaye si Myahudi). Shukrani ni za Mungu kwa kuwa hajaniumba mwanamke. Shukrani ni za Mungu kwa kuwa hajaniumba mjinga.''[4]

Hawa wa Kibiblia amechukua sehemu kubwa katika Ukristo kuliko katika Uyahudi. Dhambi yake imekuwa nitegemeo kwa imani yote ya Kikristo kwa sababu itikadi ya Kikristo juu ya sababu za kazi ya Yesu Kristo Duniani imejengwa kutokana na maasi ya Hawa wa Biblia kwa Mungu. Hawa alifanya dhambi kisha alimshawishi Adam afuate mkumbo wake. Kwa hiyo, Mungu aliwafukuza wote wawili watoke Peponi waende ardhini, ardhi ambayo imelaaniwa kwa ajili yao. Walirithisha dhambi yao, ambayo haikusamehewa na Mungu, kuwarithisha kizazi chao chote na kwa hiyo, binadamu wote wanazaliwa wakiwa na dhambi. Ili kuwatakasa wanadamu kutoka katika "dhambi zao za asili," Mungu alilazimika kumtoa muhanga msalabani, Yesu, ambaye anazingatiwa kuwa ni mwana wa Mungu. Kwa hiyo, Hawa anabeba kosa lake, dhambi ya mumewe, dhambi ya asili ya binadamu wote, na kifo cha Mwana wa Mungu. Kwa

[3]Thena Kendath, "Memories of an Orthodox youth" in Susannah Haschel ed. On being a Jewish Feminist (New York:Schocken Books, 1983), pp. 96-97.
[4] Swidler, op. cit., pp 80-81.

maneno mengine, matendo ya mwanamke mmoja kwa nafsi yake yamesababisha kuangamia kwa binadamu.[5] Je, kuna nini kwa mabinti zake? Hao nao ni wakosaji kama yeye na wanalazimika kutendewa kama alivyotendewa yeye. Sikiliza muono wa kuhuzunisha wa mtakatifu Paulo katika Agano Jipya: "*Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna. Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu. Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye. Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa." (1 Timotheo 2:11-14).*

Mt. Tertullian pia alikuwa butu mno kuliko Mt. Paulo, alipokuwa akiongea na 'watawa wake awapendao sana kiimani, alisema:[6] *"Je, hivi hamjui kuwa nyinyi nyote ni akina Hawa? Hukumu, (Maelezo) ya Mungu juu ya jinsia yenu yanaishi katika zama hizi: uovu nao lazima uwe unaishi. Nyinyi ni mlango wa Shetani: Nyinyi ndio waondoaji kizuizi cha mti ulioharamishwa: Nyinyi ndio wa mwanzo kuacha sheria takatifu: Nyinyi ndio yule mwanamke aliyemshawishi mwanamume ambaye shetani alishindwa kupata ujasiri wa*

---

5 Rosemary R. Ruether, "Christianity", in Arvind Sharma, ed., Women in World Religions (Albany State University of New York Prees, 1987) p. 209

6 For all the sayings of the Prominent Saints, see Karen Armstrong, The Gospel According to Woman (London: Elm Tree Books, 1986) pp. 52-62. See also Nancy van Vuuren, The Subversion of Women as Practiced by Churches, Witch-Hunters, and Other Sexists (Philadelphia: Westminister Press) pp. 28-30.

*kutosha kumvamia. Nyinyi ndio mlioharibu kirahisi picha ya Mungu, mwanamume. Kwa sababu ya dhambi zenu hata Mwana wa Mungu amelazimika afe.”*

Mt. Augustine alikuwa ni mwaminifu kwa waliomtangulia, alimuandikia rafiki yake: *“Hakuna tofauti kwa mwanamke awe mke au mama, ataendelea kuwa ni Hawa tu ambaye ni mshawishi kwa hiyo, lazima tujihadhari na mwanamke yeyote yule... Nimeshindwa kupata faida ya mwanamke kwa mwanamume, ukitoa tendo la kuzaa watoto.”*

Baada ya karne kadhaa, Mt. Thomas Aquinas aliendelea kuamini kuwa wanawake ni wasaliti: “Kwa mintarafu ya tabia ya kimaumbile ya kila mmoja, mwanamke ni masaliti na ni mwanaharamu, kwa nguvu iliyo hai, kwa mbegu ya mwanamume inaelekea kutoa tunda lenye kufanana kikamilifu na jinsia ya kiume; huku tunda la mwanamke linakuja kutoka katika dosari ndani ya nguvu iliyohai au kutoka katika baadhi ya malighafi mbovu, au hata kutoka baadhi ya athari za nje.”

Mwisho, mwanamageuzi mashuhuri Martin Luther hajaona faida yoyote kwa mwanamke ispokuwa kuleta watoto wengi duniani kwa kiasi kinachowezekana bila kujali athari mbaya zozote: “*Kama watachoka au kufa, hakuna tatizo. Waache wafe kwa kuzaa, kwani hiyo ndio sababu ya kuwepo kwao.”*

Tena na tena wanawake wote ni wa kuadhiriwa kwa sababu ya taswira ya Hawa ambaye ni mlaghai, shukrani zende kwa fikra iliyopo katika kitabu cha Mwanzo. Kwa muhtasari,

itikadi ya Kiyahudi-Kikristo juu ya Mwanamke imetiwa sumu kwa imani ya kuamini dhambi ya asili ya Hawa na watoto wake wa kike. Na kama, kwa sasa tutaangalia Quran inasema nini juu ya wanawake, punde tu, tutatambua kuwa itikadi ya Kiislamu juu ya mwanamke ina tofauti za kimsingi na itakadi za Kiyahudi-Kikristo. Acha Quran iongee yenyewe:

*"Bila shaka wanaume wenye kufuata vizuri nguzo za Uislamu, na wanawake wanaozifuata vizuri nguzo za Uislamu; na wanaume wanaoamini vizuri nguzo za Imani, na wanawake wanaoamini vizuri nguzo za Imani; na wanaume wanaotii, na wanawake wanaotii; na wanaume wasemao kweli, na wanawake wasemao kweli; na wanaume wanaosubiri, na wanawake wanaosubiri; na wanaume wanaonyenyekea na wanawake wanaonyenyekea; na wanaume wanaotoa (Zaka na) sadaka na wanawake wanaotoa (Zaka na) sadaka, na wanaume wanaofunga; na wanawake wanaofunga; na wanaume wanaojihifadhi tupu zao; na wanawake wanaojihifadhi; na wanaume wanaomtaja Mungu kwa wingi; na wanawake wanaomtaja Mwenyezi Mungu (kwa wingi) Mwenyezi Mungu; amewaandalia msamaha na ujira mkubwa."* (Quran 33:35)

"*Na wanaoamini wanaume na wanaoamini wanawake, ni marafiki wao kwa wao. Huyaamrisha yaliyo mema na huyakataza yaliyo mabaya na husimamisha Sala na hutoa Zaka na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao ndio*

*ambao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.* (Quran 9:71)

"*Mola wao Akawakubalia (maombi yao kwa kusema): "Hakika Mimi sitapoteza juhudi (amali) ya mfanya juhudi miongoni mwenu, akiwa mwanamume au mwanamke, (kwani nyinyi) ni nyinyi kwa nyinyi…." (Quran 3:195*).

"*Afanyaye ubaya hatalipwa ila sawa na huo uwovu wake na afanyaye mema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Mwislamu, basi hao wataingia Peponi, waruzukiwe humo bila hisabu."* (Quran 40:40)

"*Wafanyaji mema, wanaume au wanawake, hali ya kuwa ni, Waislamu Tutawahuisha maisha mema, na Tutawapa ujira wao (Akhera) mkubwa kabisa kwa sababu ya yale mema waliyokuwa wakiyatenda*. (Quran 16:97).

Ni wazi kuwa mtazamo wa Quran juu ya wanawake hauna tofauti na mtazamo wake juu ya wanaume. Wao wote, (wanawake na wanaume) ni viumbe wa Mungu ambao lengo kuu la kuletwa kwao duniani ni kumuabudu Mungu wao, kutenda matendo mema, na kujiepusha na maovu na wote wawili watalipwa kwa matendo yao. Quran haijaonyesha kuwa mwanamke ni mlango wa Shetani wala kuwa amezaliwa akiwa ni mlaghai. Quran pia, haijataja kuwa mwanamume ni sura ya Mungu; lakini wanaume wote na wanawake wote ni viumbe vya Mungu, bila ziada. Kwa mujibu wa Quran, kazi za mwanamke duniani si kuzaa watoto tu, lakini pia anatakiwa atende mema mengi kama

mwanamume anavyotakiwa afanye. Kamwe Quran haijasema kuwa hakuna mwanamke mwema aliyewahi kuishi. Kinyume chake tunaona Quran imeshawafundisha waumini wote, wake kwa waume, kufuata mfano wa wanawake wakamilifu kama vile Bikira Maria na Mke wa Firauni:

"*Na Mwenyezi Mungu amepiga (anapiga) mfano wa wale walioamini kweli, ni mkewe Firauni. (Mumewe kafiri kubwa namna hilo na yeye Mwislamu mzuri namna hivyo). (Wakumbusheni watu) aliposema: "Ee Mola wangu! Nijengee nyumba Peponi karibu yako, na Uniokoe na Firauni na amali zake (mbovu), na Niokoe na watu madhalimu." Na mariamu mtoto wa 'Imrani aliyejihifadhi nafsi yake na Tukampulizia humo roho Yetu, (inayotokana na Sisi) na akayasadikisha maneno ya Mola wake, na Vitabu vyake; na alikuwa miongoni mwa wanyenyekevu (wakubwa)*. (Quran 66:11-12)

# SEHEMU 3

# MABINTI WANAOTIA AIBU

Kwa hakika, tofauti iliyopo kati ya mtazamo wa Quran na Biblia juu ya jinsia ya kike inaanza punde tu anapozaliwa mwanamke. Kwa mfano, Biblia inaeleza kuwa kipindi cha mama aliyezaa cha kuwa si msafi kwa mujibu wa sheria za kidini ni mara mbili ya urefu wa kawaida ikiwa mtoto atakuwa mwanamke kinyume na mwanamume. (Mambo ya Walawi 12:2-5). Biblia ya Kikatoliki inaeleza kikamilifu kuwa: "*Kuzaliwa kwa binti ni hasara*" (Ecclesiasticus 22:3). Kinyume cha maelezo haya yanayotia mshtuko na kupaza roho, watoto wa kiume wanapokea sifa za kipee: "*Mwenamume anayemuelimisha mwanawe wa kiume atahusudiwa na maadui zake*." (Ecclesiasticus 30:3).

Wanazuoni wa Kiyahudi wameamrisha Wayahudi wa kiume wazaliane watoto wengi ili waendeleze kabila la Kiyahudi. Wakati huo huo, hawafichi upendeleo wao wa wazi kwa watoto wa kiume: "*Ni uzuri kwa wale wote ambao watoto wao ni wa kiume lakini ni ubaya kwa wale wote ambao watoto wao ni wanawake", "Anapozaliwa mtoto wa kiume, watu wote wanashangilia.... na anapozaliwa mtoto wa kike*

*watu wote wanahuzunika"* na *"wakati mtoto wa kiume anapokuja duniani, amani inakuja duniani… Wakati mtoto wa kike anapokuja duniani, hakuna kitu kinachokuja*."[7]

Binti anazingatiwa kuwa ni mzigo mzito, chanzo cha uwezekano wa aibu kwa baba yake: *"Binti yako ni mkaidi? Jihadhari ya kwamba asije akawachekesha maadui zako, Na uwe gumzo la watu mji mzima, mada ya udaku wa kawaida, na atakutia aibu mbele za watu." (Ecclesiasticus 42:11). "Lazima uwe mkali na binti mkaidi, au vinginevyo atatumia vibaya kumdekeza kwako. Mchunge vikali Sana katika macho yake yasiyo na aibu, usishangae kama atakuletea aibu."* (Ecclesiasticus 26:10-11).

Ilikuwa ni fikra ile ile ya kuwatendea mabinti kwa mtazamo wa kuwa wao ndio chanzo cha aibu ambayo iliwapelekea wapagani wa Kiarabu, kabla ya kuja kwa Uislamu, kuwafanyia wanawake mauaji wangali wachanga.

Quran imelaani vikali mno tendo hilo la kuchukiza: *"(Akawa) anajificha na watu kwa sababu ya khabari mbaya ile aliyoambiwa! (Anafanya shauri!) Je, akae naye juu ya fedheha hiyo au amfukie udongoni (kaburini, na hali ya kuwa mzima ili afe?) Sikilizeni! Ni mbaya mno hukumu yao hiyo." (Quran 16:59).*

---

[7] Swidler, op. cit., p. 140

Ni lazima ionyeshwe kuwa uovu huu usingekoma katika bara Arabu kama kusingekuwa na nguvu za matamamko makali ya Quran ambayo yalilaani matendo hayo. (Quran 16:59, 43:17, 81:8-9). Quran, juu ya hayo, haifanyi ubaguzi kati ya wavulana na wasichana. Kinyume na Biblia, Quran inazingatia kuwa kuzaa mtoto wa kike ni zawadi na baraka kutoka kwa Mungu, na hivyo hivyo katika kuzaa mtoto wa kiume. Pia Quran imetanguliza kutaja zawadi ya kuanza kuzaa mtoto wa kike: "*Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu; Anaumba Apendavyo, Anampa Amtakaye watoto wa kike na Anampa Amtakaye watoto wa kiume*". (Quran 42:49).

Ili kukomesha kabisa kabisa matendo yote ya kuwaangamiza wanawake mwanzoni mwa jamii ya Kiislamu, Mtume Muhammad (S.A.W) aliwaahidi wale wote waliobarikiwa kuzaa watoto wa kike kuwa watapata thawabu kubwa kama watawalea vizuri: "*Yoyote atakayemlea mtoto wa kike, na kwa mujibu wa kuwatendea wema watoto hao, watoto hao watamkinga baba yao dhidi ya Moto wa Jahannamu*" (Bukhari na Muslim), "*Yoyote atakayewalea watoto wawili wa kike hadi wakakua, mimi na yeye tutakuwa kama hivi siku ya Kiyama; na aliashiria kwa kuvibana pamoja vidole (akimaanisha kuwa watakuwa pamoja)*. (Imepokelewa na Muslim).

# SEHEMU 4

# ELIMU KWA WANAWAKE

Tofauti iliyopo kati ya itikadi ya Biblia na ya Quran juu ya wanawake haijafungika katika kuzaa tu mtoto wa kike, lakini inaendelea na kupanuka kwa upeo mkubwa sana kuliko hivyo. Hebu acha tulinganishe mitazamo ya vitabu hivyo juu ya majaribio ya mtoto wa kike kujifunza dini yake. Moyo wa Uyahudi ni Torati, ambayao ni sheria. Hata hivyo, kulingana na kitabu Talmudi, (kitabu muhimu sana kwa Wayahudi), inasema: *"wanawake hawaruhusiwi kujifunza Torati."* Baadhi ya wanazuoni wa Kiyahudi kwa ukali wametangaza kuwa *"ni bora kuyaacha maneno ya Torati yaunguzwe moto kuliko kusomwa na mwanamke"* na *"Yeyote atakayemfundisha Torati binti yake amemfundisha uchafu*."[8]

Mtazamo wa Mt. Paulo katika Agano Jipya haupo wazi: "W*anawake na wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena; bali watii, kama vile inenavyo Torati nayo. Nao wakitaka kujifunza neno lo lote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu wanawake kunena katika kanisa*." (Wakorintho wa Kwanza 14:34-35)

---

[8]Denise L. Carmody, "Judaism", in Arvind Sharma, ed., op. cit., p. 197.

Vipi mwanamke ataweza kujifunza ikiwa haruhusiwi kuongea? Vipi mwanamke atakua kiakili ikiwa amelazimishwa kuwa katika hali ya utiifu kikamilifu? Vipi mwanamke ataweza kujipanua upeo wake wa kielimu ikiwa chanzo chake cha pekee cha kupata elimu ni mumewe tu akiwa nyumbani?

Sasa, ili tuwe waadilifu, tunapaswa tuulize: Je, nafasi ya Quran ina tofauti yeyote? Moja ya habari fupi iliyosimuliwa ndani ya Quran inataja nafasi yake kwa ufahamu wa kina zaidi. Bibi Khawlah alikuwa ni mwanamke wa Kiislamu ambae mumewe bwana Awsi alipokuwa na hasira alimtamkia maneno haya: "*Wewe kwangu mimi ni sawa na mgongo wa mama yangu*." Jambo hilo lilikuwa likichukuliwa na wapagani wa Kiarabu kuwa ni maneno ya talaka ambayo inamuacha huru mume, asitende mambo yote ya unyumba yanayomlazimu lakini hayamuachi huyo mwanamke huru aiache nyumba ya mume au aolewe na mtu mwingine. Aliposikia maneno hayo kutoka kwa mumewe, Khawlah akawa na wakati mgumu sana. Bibi huyo akaenda moja kwa moja hadi kwa Mtume wa Uislamu ili kutetea kesi yake. Mtume (S.A.W) alikuwa na rai ya kumtaka bibi huyo awe mtulivu kwa kuwa hakuna njia ya kutatua tatizo hilo kwa wakati huo. Khawlah akaendelea kujadiliana na Mtume (S.A.W) akijaribu kuokoa ndoa yake iliyotundikwa. Punde tu, Quran ikaingilia kati; na maombi ya Khawlah yakakubaliwa. Hukumu takatifu ikakomesha tabia hiyo mbaya sana. Sura moja kamilifu (sura ya 58) ya Quran

inaitwa "*Almujadilah"* au "*mwanamke ambaye amefanya mjadala*" iliitwa hivyo kwa ajili ya tukio hilo:

"*Mwenyezi Mungu amekwishasikia usemi wa mwanamke yule anayejadiliana nawe sababu ya mumewe, na anashtaki mbele ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu anayasikia majibizano yenu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kuona.*" (Quran 58:1)

Mwanamke katika itikadi ya Quran anayo haki ya kupinga rai, hata kama ni rai ya Mtume wa Uislam (S.A.W). Hakuna mwenye haki ya kumnyamazisha Mwanamke. Mwanamke hayupo chini ya amri ya kumtaka mumemewe awe ndiye marejeo yake ya pekee katika masuala ya kisheria na kidini.

# SEHEMU 5

# MWANAMKE MWENYE HEDHI SI MSAFI

Sheria na hukumu za Kiyahudi juu ya hedhi ya wanawake ni kali mno. Agano la kale linamchukulia mwanamke yeyote mwenye hedhi kuwa si msafi na ni najisi. Zaidi ya hayo unajisi wake "*unaambukiza*" wenginewe vile vile. Mtu yeyote au kitu chochote atakachokigusa kitanajisika kwa siku nzima: "*Mwanamke ye yote, kama anatokwa na kitu, na kitu chake alichokuwa nacho mwilini mwake ni damu, ataketi katika kutengwa kwake muda wa siku saba; na mtu ye yote atakayemgusa atakuwa najisi hata jioni. Na kitu cho chote akilaliacho katika kutengwa kwake kitakuwa najisi; na kila kitu ambacho akiketia kitakuwa najisi. Mtu ye yote atakayekigusa kitanda chake huyo mwanamke atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa najisi hata jioni. Mtu yeyote atakayekigusa cho chote ambacho huyo mwanamke amekiketia atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa najisi hata jioni. Kwamba ni katika kitanda, au cho chote alichokilalia huyo mwanamke, atakapokigusa kitu hicho, atakuwa najisi hata jioni*". (Law. 15:19-23).

Kwa sababu ya maumbile yake ya "kutia najisi"; mwanamke mwenye hedhi mara nyingine alipelekwa uhamishoni ili kuepusha uwezekano wowote wa kukutana naye. Hupelekwa nyumba maalumu ziitwazo "nyumba ya wasio wasafi" kwa kipindi chote cha hedhi yake.[9] Talmudi inamchukulia mwanake mwenye hedhi ni "mauti" hata kama hakuna mafungamano ya kimwili: *"Walimu zetu wa dini ya Kiyahudi wametufunza... kama mwanamke mwenye hedhi atapita kati ya (wanaume) wawili, ikiwa ni mwanzoni mwa hedhi yake, mwanamke huyo atamnyonga mmoja wao, na kama akiwa mwishoni mwa hedhi yake, atasababisha ugomvi kati ya wanaume hao*." (Bpes.111a.)

Zaidi ya hayo, mume wa mwanamke mwenye hedhi alizuiwa kuingia sinagogini kama atachafuliwa na mkewe tena hata kwa mavumbi yaliyo chini ya miguu yake. Kasisi yeyote ambaye mkewe, bintiye, au mamaye ni mwenye hedhi hakuruhusiwa kuhubiri baraka sinagogini.[10] Si ajabu kuwa wanawake wengi wa Kiyahudi wanaendelea kuona kuwa hedhi ni "*laana*."[11]

Uislamu hauoni kuwa mwanamke mwenye hedhi ana aina yoyote ya "*najisi ya kuambukiza kwa kugusana*". Mwanamke mwenye hedhi si mtu wa "*kutoguswa*" wala "*laana.*"

---

[9] Swidler, op. cit., p. 137.
[10] Ibid., p 138.
[11] Sally Priesand, Judaism and the New Woman (New York: Behraman House, Inc., 1975) p.24.

Mwanamke huyo anafanya shughuli zake za kawaida huku kukiwa na jambo moja tu linalotolewa: Kwa wale walioolewa hawaruhusiwi kutenda tendo la ndoa wakiwa katika kipindi cha hedhi. Lakini matendo mengine yote ya kugusana kimwili baina yao yanaruhusiwa. Mwanamke mwenye hedhi amekatazwa asitende baadhi ya ibada kama vile sala za kila siku, na kufunga akiwa katika kipindi cha hedhi.

# SEHEMU 6

# HAKI YA KUTOA USHAHIDI

Kadhia nyingine ambayo Quran na Biblia hazikubaliani ni kadhia ya mwanamke kutoa ushahidi. Ni kweli kuwa Quran imewafunza waumini ambao wanashughulika na mikataba ya kibiashara wawe na mashahidi wawili wa kiume au mwanamume mmoja na wanawake wawili (Quran 2:282). Hata hivyo, ni kweli kwamba Quran katika matukio mengine inakubali ushahidi wa mwanamke ukiwa ni sawa sawa na wa mwanamume. Na kwa hakika ushahidi wa mwanamke unaweza ukawa ni bora zaidi kuliko wa mwanamume. Na kama mwanamume atamtuhumu mkewe kuwa anafanya uzinzi, mwanamume huyo anatakiwa na Quran aape kiapo cha dhati mara tano hii ikiwa ni kama ushahidi wa kuwa mke ni muovu. Na kama mke atapinga na kuapa kama hivyo mara tano, mwanamke huyo hazingatiwi kuwa ni muovu na kwa hali yoyote likitokea jambo hilo ndoa itavunjwa. (Quran 24:6-11)

Kwa upande mwingine, katika jamii za kale za Kiyahudi wanawake hawakuruhusiwa kutoa ushahidi.[12] Wanazuoni wa Kiyahudi waliwahesabu wanawake kuwa hawawezi kutoa ushahidi. Jambo hilo ni miongoni mwa laana tisa zinazowatesa wanawake wote kwa sababu ya “kuporomoka” (tazama sehemu ya *Urithi wa Hawa)*. Katika Israeli ya leo, wanawake hawaruhusiwi kutoa ushahidi katika mahakama za kidini.[13] Wanazuoni wanahalalisha sababu za kutoruhusiwa kwa wanawake kutoa ushahidi kwa kukariri (Mwanzo 18:9-16), pale ilipoeleza kuwa Sara mke wa Ibrahimu ameongopa. Wanazuoni wa Kiyahudi wanatumia tukio hili kama ni ushahidi wa kuwa wanawake hawana vigezo vya kuwa mashahidi. Hapa inapaswa izingatiwe kuwa, kisa hiki kilichosimuliwa na Mwanzo 18:9-16 kimetajwa zaidi ya mara moja katika Quran bila ya kudokeza kama Sara aliongopa. (Quran 11:69-74, 51:24-30). Katika Ukristo wa Kimagharibi, vyanzo viwili Ecclesiastical na sheria ya uraia viliwakataza wanawake wasitoe ushahidi hadi mwishoni mwa karne iliyopita.[14]

Kama mwanmume atamtuhumu mkewe kwa uzinzi, ushahidi wa mwanamke huyo hautokubaliwa kabisa kabisa kwa mujibu wa Biblia. Mke anayetuhumiwa lazima akabiliwe na

[12] Swidler, op. cit., p. 115
[13] Lesley Hazleton, Israel Women The Reality Behind the Myths (New York: Simon and Schuster, 1977) p. 41.
[14] Gage, op. cit. p. 142

hukumu ya kuchunguzwa kwa kuteswa. Katika majaribio hayo, mke atakabiliwa na kanuni za kidini zikichanganyika na kufedheheshwa ambazo zitapendekezwa ili kuthibitisha uovu wake au utakatifu wake. (Hesabu 5:11-31). Na kama atapatikana na hatia baada ya kuchunguzwa kimateso, mwanamke huyo atahukumiwa kifo. Na kama itagundulika si muovu, mumewe atakuwa hana hatia yoyote ya kumtendea vibaya.

Licha ya hayo, kama mwanamume atamuoa mwanamke kisha akamtuhumu kuwa si bikira, ushahidi wa mwanamke huyo hautokubaliwa. Wazazi wake watalazimika kuleta ushahidi wa ubikira wake mbele ya wazee wa mji. Na kama wazazi watashindwa kuleta ushahidi wa kuthibitisha utakatifu wa binti yao, binti huyo atapigwa mawe hadi afe mlangoni katika ngazi za nyumba ya babaye. Na kama wazazi wataweza kuthibitisha utakatifu wake, yule mume atapigwa faini tu; ya shekeli za fedha mia moja na mume huyo haruhusiwi kumuacha mke huyo maisha:

"*Mtu akitwaa mke, akamwingilia na kumchukia, kisha akimshitaki mambo ya aibu kumzushia jina baya, akasema, Nimemtwaa mwanamke huyu, nami nilipomkaribia sikuona kwake alama za ubikira; ndipo babaye yule kijana na mamaye watakapotwaa alama za yule kijana za ubikira, wawatolee wazee wa mji langoni; na baba yake yule kijana awaambie wazee, Mwanamume huyu nilimpa binti yangu awe mkewe, naye amchukia; angalieni amemwekea mambo ya aibu, asema, Sikuona kwa binti yako alama za ubikira,*

*nazo hizi ndizo alama za binti yangu za ubikira. Na wayakunjue yale mavazi mbele ya wazee wa mji. Basi wazee wa mji ule na wamtwae yule mtu mume na kumrudi, wamtoze shekeli mia za fedha, wampe babaye yule kijana, kwa kuwa amemzulia jina baya mwanamwali wa Israeli; naye awe mkewe; hana ruhusa ya kumuacha siku zake zote. Lakini likiwa ni kweli neno hili, la kutoonekana kwake yule kijana alama za ubikira, na wamtoe nje yule kijana mlangoni pa nyumba ya baba yake, na waume wa mji wake wampige kwa mawe hata afe; kwa vile alivyofanya upumbavu katika Israel, kwa kufanya ukahaba katika nyumba ya baba yake; ndivyo utakavyoondo uovu katikati yako*. (Kum. 22:13-21).

# SEHEMU 7

# UASHERATI

Uzinzi unazingatiwa kuwa ni dhambi katika dini zote. Biblia inatangaza adhabu ya kifo kwa wote wawili mzinifu mwanamume na mzinifu mwanamke (Law. 20:10). Uislam pia unatoa adhabu iliyo sawa kwa wote wawili mzinifu mwanamume na mzinifu mwanamke (Quran 24:2). Hata hivyo, ufafanuzi wa Quran juu ya uzinzi una tofauti sana na ufafanuzi wa Biblia. Uzinzi, kwa mujibu wa Quran, ni kushiriki tendo la ngono nje ya ndoa kwa aliyeoa au aliyeolewa. Lakini Biblia inazingatia tendo la ngono nje ya ndoa kuwa ni uzinzi kwa mwanamke aliyeolewa. (Law. 20:10, Kum 22:22, Methali 6:20-7:27).

"Akifumaniwa mtu mume amelala na mwanamke aliyeolewa na mume, na wafe wote wawili, mtu mume alielala na mwanamke, na yule mwanamke naye; ndivyo utakavyoondoa uovu katika Israeli. (Kum 22:22)

"*Na mtu aziniye na mke wa mtu mwingine, naam, yeye aziniye na mke wa jirani yake, mtu mume aziniye, na mwanamke aziniye, hakika watauawa*. (Law. 20:10).

Kwa mujibu wa ufafanuzi wa Biblia, kama mwanamume aliyeoa atalala na mwanamke asiyeolewa, jambo hilo halichukuliwi kuwa ni uovu kabisa kabisa. Mwanamume aliyeoa anayefanya ngono nje ya ndoa na mwanamke asiyeolewa si mzinzi na mwanamke asiyeolewa aliezini naye, pia, si mzinzi. Uovu wa zinaa unatendeka pale tu, mwanamume aliyeoa au asiyeoa, anapolala na mwanamke aliyeolewa. Kwa hali hii mwanamume anachukuliwa kuwa ni mzinifu, hata kama hajaoa, na mwanamke anachukuliwa kuwa ni mzinifu. Kwa ufupi, uzinzi ni uovu wa kingono unaomuhusisha mwanake aliyeolewa. Matendo ya ngono nje ya ndoa yanayomuhusu mwanamume aliyeoa si uzinzi kwa mujibu wa Biblia. Kwa nini huu undumilakuwili? Kwa mujibu Insaiklopidia ya Kiyahudi, mke anazingatiwa kuwa ni miliki ya mume na uzinzi unatoa madaraka ya uvunjaji wa sheria kumvunjia mume kwa haki ya kipekee aliyonayo kwa mwanamke; mke kama miliki ya mume hana haki kama hiyo kwa mumewe.[15] Hiyo ndio maana, kama mwanamume atafanya ngono na mwanamke aliyeolewa, mwanamume huyo atakuwa amevunja mali ya mwanamume mwingine na, kwa hiyo lazima aadhibiwe.

Hadi hivi leo katika nchi ya Israeli, kama mwanamume aliyeoa atajitumbukiza katika ngono nje ya ndoa na mwanamke asiyeolewa, watoto wake kwa mwanamke huyo

[15] Jeffrey H. Togay, "Adultery," Encyclopaedia Judaica, Vol. 2, col. 313. Also, see Judith Plaskow, Standing Again at Sinai: Judaism from a Feminist Perspective (New York: Harper & Row Publishers, 1990) pp. 170-177.

wanazingatiwa kuwa ni watoto wa halali wa ndoa. Lakini, kama mwanamke aliyeolewa atafanya ngono nje ya ndoa na mwanamume mwingine (si mumewe) aliyeoa au asiyeoa, watoto wake kwa mwanamume huyo si wa halali tu lakini pia wanazingatiwa kuwa ni watoto wa haramu na ni haramu kwa watoto huo kuoa au kuolewa na Myahudi yeyote ispokuwa aliyeitoka dini ya Kiyahudi na watoto wa nje ya ndoa wengine. Katazo hili linaendelea kwa vizazi vya mtoto huyo kwa madaraja ya vizazi 10 mpaka uvundo wa uzinzi uthibitishwe kufifia.[16]

Quran, kwa upande mwingine, kamwe haijamzingatia mwanamke yeyote kuwa ni mmilikiwa na mwanamume yeyote. Quran kiuadilifu anaelezea uhusiano kati ya mume na mke kwa kusema:

"*Na katika Ishara zake (za kuonyesha ihsani Zake juu yenu) ni kuwa Amekuumbieni wake zenu katika jinsi yenu ili mupate utulivu kwao, naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Bila shaka katika haya zimo Ishara kwa watu wanaofikiria.*" (Quran 30:21).

Hii ndiyo itikadi ya Quran juu ya ndoa; mapenzi, huruma, na utulivu, raha, na sio miliki na undumilakuwili.

---

[16] Hazleton, op. cit., pp. 41-42.

# SEHEMU 8

# KULA KIAPO NA KUWEKA NADHIRI

Kwa mujibu wa Biblia, mwanamume lazima atimize kila nadhiri na kiapo alichoapa kwa Mungu. Haramu kugeuza neno lake. Kwa upande mwingine, nadhiri au kiapo cha mwanamke hakilazimiki kwake. Nadhiri au kiapo cha mwanamke lazima kitimizwe na baba yake, kama atakuwa anaishi kwenye nyumba ya baba yake, au atimiziwe na mumewe, akiwa ameolewa. Kama baba/mume hajaidhinisha nadhiri ama kiapo cha binti yake au mkewe, viapo, ahadi, nadhiri na dhamana zote zilizofanywa na mwanamke huyo zinakuwa ni batili na ni kazi bure:

"*Lakini kama huyo baba yake akimkataza siku hiyo aliyosikia; nadhiri zake ziwazo zote, wala vifungo vyake alivyoifungia nafsi yake havitathibitika....*" *Na mumewe alisikia akamnyamazia, wala hakumkataza; ndipo nadhiri Zake zote zitathibitika na kila kifungo alichofunga kitathibitika*. (Hesabu 30:5-15).

Kwa nini iwe maneno ya mwanamke hayashurutishwi kwake? Jibu ni lepesi: Ni kwa sababu mwanamke

anamilikiwa na baba yake, kabla ya kuolewa, au na mumewe baada ya kuolewa. Utawala wa baba kwa binti yake ulikuwa ni dhahiri kwa upeo ambao, kama atataka, anaweza kumuuza! Na jambo hilo limeonyeshwa katika maandiko ya wanazuoni wa Kiyahudi kuwa: *"Mwanamume anaweza kumuuza binti yake, lakini mwanamke hawezi kumuuza binti yake, Mwanamume anaweza kumchumbia binti yake, lakini mwanamke hawezi kumchumbia binti yake*."[17] Mafundisho ya wanazuoni wa Kiyahudi, vile vile yanaonyesha kuwa ndoa inawakilisha ahamishaji wa utawala toka kwa baba kwenda kwa mume: *"Uchumba, unamfanya mwanamke awe miliki tukufu sana ... mali isiyokiukwa kwa mume*…." Ni wazi, kama mwanamke anahesabiwa kuwa ni mali ya mtu mwingine, mwanamke huyo hatoweza kula kiapo chochote ambacho hakitathibitishwa na mmiliki wake.

Ni muhimu kuona kuwa Jambo hili la mafundisho ya Biblia kuhusu viapo vya mwanamke limeendelea kuathiri vibaya nafasi ya wanawake katika itikadi ya Kiyahudi-Kikristo hadi mwanzoni mwa karne hii. Mwanamke aliyeolewa katika ulimwengu wa Kimagharibi hana hali ya uhalali wa nafsi yake. Hakuna tendo la mwanamke lenye thamani yoyote kisheria. Mumewe anaweza kukana mkataba wowote; mapatano ya kibiashara, au mpango wowote alioufanya. Wanawake katika nchi za Kimagharibi (eneo kuu lilorithi mtazamo wa Kiyahudi-Kikristo) hawawezi kuweka masharti

[17] Swidler, op. cit., p. 141.

yoyote ya kimikataba kwa sababu wanawake hao wanamilikiwa na watu wengine. Wanawake wa Kimagharibi walitaabika kwa takriban miaka elfu mbili, kwa sababu ya mtazamo wa Biblia juu ya nafasi ya wanawake kwa baba zao na kwa waume zao.[18] Katika Uislamu, kiapo cha kila Mwislamu, mwanamume au mwanamke, anashurutishwa kwa nafsi yake mwenyewe. Hakuna mtu mwenye madaraka ya kukana kiapo cha mtu mwingine yeyote.

Kushindwa kutekeleza kiapo ipasavyo, kilichoapwa na mwanamume au mwanamke, ni lazima alipe fidia kama ilivyotajwa katika Quran:

"*Mwenyezi Mungu hatakuteseni kwa viapo vyenu vya upuuzi, lakini Atakukamateni kwa viapo mlivyoapa kwa nia mliyoifunga barabara. Basi kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha katikati mnachowalisha watu wa majumbani mwenu, au kuwavisha, au kumpa uungwana mtumwa, Lakini asiyeweza kupata hayo, basi afunge siku tatu. Hii ndio kafara ya viapo vyenu mnapoapa. Na vilindeni viapo vyenu, (msiape kisha msitimize). Namna hii Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya Zake ili mpate kushukuru.*" (Quran 5:89)

Wafuasi wa Mtume Muhammad (S.A.W) waume kwa wake, walikuwa wakiwasilisha viapo vyao vya kumtii, wao

[18] Matilda J. Gage, Woman, Church, and State (New York: Truth Seeker Company, 1893) p. 141.

wenyewe. Wanawake, sawa na wanaume, walikuwa wanamuendea Mtume kila mtu mwenyewe na kula viapo vyao.

"*Ewe Nabii! Watakapokujia wanawake walioamini wanakuahidi ya kwamba hawatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote, wala hawataiba, wala hawatazini, wala hawatawaua watoto wao, wala hawataleta uzushi wanaouzusha tu wenyewe baina ya mikono yao na miguu yao, wala hawatakuasi katika jambo jema, basi peana ahadi nao na uwatakie maghufira kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwingi wa rehema*." (Quran 60:12)

Mwanamume haruhusiwi kula kiapo kwa niaba ya binti yake au mkewe. Wala hawezi kukana kiapo cha yeyote miongoni mwa jamaa zake wa kike.

# SEHEMU 9

# MALI ZA MKE

Hizi dini tatu zinashirikiana katika imani isiyo na mashaka kuhusu umuhimu wa ndoa na maisha ya kifamilia. Pia zinakubaliana katika suala la kumpa mwanamume uongozi wa familia. Bila ya kujali, tofauti za wazi zilizopo kati ya dini hizo tatu, pamoja na kuheshimu mipaka ya uongozi. Mafundisho ya Kiyahudi-Kikristo hayafanani na ya Uislamu, katika ukweli wa upeo wa uongozi wa mume hadi kufikia umiliki wa mume kummiliki mkewe.

Mafundisho ya Kiyahudi yanalichukulia jukumu la mume kwa mkewe kuwa linaanzia kutoka katika itikadi ya kuamini kuwa mume anammiliki mke kama anavyomiliki mtumwa wake.[19] Itikadi hii imekuwa hoja nyuma ya undumilakuwili katika sheria ya uzinzi na nyuma ya uwezo wa mwanamume wa kubatilisha viapo vya mkewe. Itikadi hii pia inahusika katika kumzuia mke asisimamie mali yake au mapato yake. Mwanamke wa Kiyahudi mara tu anapoolewa, mwanamke huyo anapoteza kabisa kabisa usimamizi wa mali zake na mapato yake, na kuchukuliwa na mumewe. Wanazuoni wa

[19] Louis M. Epstein, The Jewish Marriage Contract (New York: Arno Press, 1973) p. 149.

Kiyahudi wanatetea haki ya mwanamume kwa mali ya mkewe kama ni matokeo ya kummiliki kwake mke huyo: "*Mtu anapokuwa mmiliki wa mwanamke je, jambo hilo halipelekei kuwa mtu huyo atakuwa mmiliki wa mali za mwanamke huyo vile vile?*" na "*Na mwanamume ajitwalie mwanamke je, hatajitwalia mali za mwanamke huyo vile vile?*[20] Kwa hiyo, ndoa imesababisha mwanamke tajiri sana awe hana kitu! Talmudi inachambua hali ya kiuchumi ya mwanamke kama ifuatavyo:

"*Vipi mwanamke awe na chochote; chochote ambacho ni chake kinamilikiwa na mumewe? Kwa mume kile ambacho ni chake basi hicho ni chake na kwa mwanamke kile ambacho ni chake basi hicho ni cha mwanamume vile vile... Pato la mwanamke na chochote atakachokipata mitaani ni cha mumewe vile vile. Vitu vya nyumbani hata kipande cha mkate juu ya meza ni vya mume. Kama atamualika mgeni nyumbani kwake na kumlisha, atakuwa anamuibia mumewe ...*" (san. 71a, Git.Ra).

Ukweli wa mambo ni kwamba mali za mwanamke wa Kiyahudi zina maana ya kuwavutia wachumba. Familia ya Kiyahudi inatoa fungu la binti yao katika kiwanja/shamba la baba yake litumiwe kama mahari atoayo mke ili aolewe. Mahari hiyo ndiyo sababu iliyowafanya mabinti wa Kiyahudi wewe ni balaa lisilotakiwa kwa baba zao. Baba analazimika

---

[20] Swidler, op. cit., p. 142.

kumlea binti yake kwa miaka mingi kisha aandae ndoa yake kwa kutoa mahari kubwa. Kwa hiyo, msichana katika familia ya Kiyahudi amekuwa ni dhima isiyo na kikomo na sio rasilimali.[21] Dhima hii isiyo na kikomo inafafanua kwa nini kuzaa binti ilikuwa si furaha na shangwe katika jamii za Kiyahudi za zamani (tazama sehemu; "*Mabinti wanaotia aibu*"). Mahari ilikuwa ni zawadi apewayo bwana harusi ili iwe milki yake chini ya sheria ya mpango wa maisha. Mume anakuwa ni mmiliki halisi wa mahari lakini haruhusiwi kuiuza. Bibi harusi anapoteza madaraka yote juu ya mahari katika kipindi cha ndoa. Zaidi ya hayo, mwanamke anatarajiwa afanye kazi baada ya kuolewa na pato lake lote lazima liende kwa mumewe ikiwa ni malipo ya huduma za lazima ambazo bibi huyo anazipata kutoka kwa mumewe. Mwanamke huyo anaweza kurudisha mali zake katika hali mbili tu: Talaka au kifo cha mumewe. Na kama mke akifa kwanza, mume anarithi mali zake. Na katika hali ya kufa kwa mume mke anarudishiwa mali zake za kabla ya ndoa lakini hajatajwa kama anarithi fungu lolote katika mali za mumewe aliyefariki. Ni lazima iongezwe kuwa mume vile vile analazimika atoe mahari kwa bibi harusi, lakini kwa mara nyingine tena mume huyo huyo ndio mmiliki halali wa zawadi hiyo kwa muda wote wa ndoa yao.[22]

[21] Epstein, op. cit., pp. 164-165.
[22] Ibid., pp. 112-113. See also Priesand, op. cit., p. 15.

Ukristo, hadi hivi karibuni, umekuwa unafuata mafundisho yale yale ya Kiyahudi. Zote mbili dini na mamlaka za sheria za raia katika himaya ya Ukristo wa Kiroma (baada ya Constantine) zinaomba maafikiano ya mali kama ni sharti la kutambuliwa kwa ndoa. Familia zinawapa mabinti zao mahari za ziada kama matokeo ya sheria hiyo. Wanaume wananuia kuoa mapema huku familia za mabinti zikichelewesha ndoa za mabinti zao kuliko kawaida.[23] Chini ya sheria ya urai, mke ametajwa kuwa anarudishiwa mahari yake kama ndoa imebatilishwa, ila kama mwanamke huyo ni mzinzi, katika hali hii, mwanamke huyo ananyang`anywa haki yake ya mahari ambayo imesalia kuwa mikononi mwa mumewe.[24] Chini ya sheria ya kanuni na sheria ya uraia mwanamke aliyeolewa katika dini ya Ukristo wa Ulaya na Marekani ameshapoteza haki za mali zake, hali hii ilikuwa inaendelea hadi mwishoni mwa karne ya kumi na tisa na mwanzoni mwa karne ya ishirini. Kwa mfano, haki za wanawake chini ya sheria ya Uingereza zilizotungwa na kuchapishwa 1632. Miongoni mwa haki hizo ni: *"Cha mume ni chake. Na cha mke ni cha mumewe*."[25] Mke sio tu anapoteza mali zake katika ndoa, pia anapoteza utu wake. Tendo lolote la mwanamke lilikuwa halina thamani yeyote

[23] James A. Brundage, Law, Sex, and Christian Society in Medieval Europe (Chicago: University of Chicago Press, 1987) p.88.
[24] Ibid., p. 480.
[25] R. Thompson, Women in Stuart England and America (London: Routledge & Kegan Paul, 1974) p. 161.

kisheria. Mumewe anaweza kubatilisha uuzaji au zawadi iliyotolewa na mke kwa kuwa haina sharti lenye thamani kisheria. Mtu yeyote atakayeingia mkataba na mke wa mtu anachukuliwa kuwa ni haramia kwa kushiriki katika ulaghai. Zaidi ya hayo, mwanamke hawezi kushtaki au kushtakiwa kwa jina lake mwenyewe, wala hawezi kumshitaki mumewe.[26] Mwanamke aliyeolewa alikuwa anatendewa kama vile ni mtoto mchanga katika jicho la sheria. Kirahisi kabisa, mke alimilikiwa na mumewe na kwa hiyo anapoteza mali zake, utu wake kisheria, na jina lake la kifamilia.[27]

Tangu karne ya saba C.E., (baada ya kuzaliwa Yesu) Uislamu umewapa wanawake waliolewa uhuru binafsi ambao Uyahudi-Ukristo wa Kimagharibi umewanyima hadi hivi karibuni tu! Katika Uislamu, bibi harusi na familia yake hawalazimishwi kutoa kitu chochote kiwe kama mahari ya kumpa bwana harusi. Msichana katika familia ya Kiislamu si dhima isiyo na kikomo. Mwanamke ana heshima kubwa sana katika Uislamu kiasi cha kutotakiwa atoe zawadi yoyote ya kumvutia mumewe mtarajiwa. Ispokuwa bwana harusi ni lazima atoe mahari ya ndoa kumpa bibi harusi. Na mahari hiyo inahesabiwa kuwa ni mali ya mke na si ya mume wala familia ya bibi harusi haina fungu au haimiliki mahari hiyo. Katika baadhi ya jamii za Kiislamu hivi sasa ni kawaida

[26] Mary Murray, The Law of the Father (London: Routlendge, 1995) p.67.
[27] Gage, op. cit., p.143.

mahari kufikia lukiki za Dola za Kimarekani, na almasi.[28] Mke anamiliki mahari yake hata kama ataachwa hapo baadaye. Mume haruhusiwi kutumia mali ya mkewe ispokuwa ile apewayo na mkewe kwa ridhaa yake mwenyewe.[29] Quran imeelezea msimamo wake juu ya mada hii kwa uwazi kabisa:

"*Na wapeni wanawake mahari yao, hali ya kuwa ni hadiya (aliyowapa Mungu). (Lakini hao wake zenu) wakikupeni kwa radhi ya nafsi zao kitu katika hayo (mahari) basi kuleni kwa furaha na kunufaika*. (Quran 4:4)

Mali na pato la mke vipo chini ya utawala wake kikamilifu na ni kwa ajili ya matumizi yake peke yake, na mutumizi ya watoto, ni jukumu la mumewe.[30] Bila kujali huyo mke ni tajiri kiasi gani, mwanamke halazimishwi kuwa mchumiaji mwenza wa mwanamume kuihudumia familia ispokuwa kama atajitolea mwenyewe na kuamua kufanya hivyo. Wanandoa wanarithiana. Zaidi ya hayo, mke katika Uislamu anamiliki uhuru wa utu wake kisheria pia na jina lake la

[28] For example, see Jeffrey Lang, Struggling to Surrender, (Beltsville, MD: Amana Publications, 1994), p. 167.

[29] Elsayyed Sabiq, Figh al Sunnah (Cairo: Darul Fatah Lile`lam Al-Arabi, 11th edition, 1994), vol. 2, pp. 218-229.

[30] Abdel-Haleem Abu Shuqqa, Tahreer al Mar`aa fi Asr al Rasala (Kuwait: Dar al Qalam, 1990) pp. 109-112.

ukoo.[31] Jaji mmoja wa Kimarekani, mara moja alitoa maelezo juu ya haki za wanawake wa Kiislamu kwa kusema: “Msichana wa Kiislamu anaweza kuolewa mara kumi, lakini uhuru wake haunyonywi kwa kufanya hivyo yaani na waume zake mbalimbali. Mwanamke wa Kiislamu ni sayari katika mfumo wa jua akiwa na jina na utu wake mwenyewe wa kisheria.[32]

[31] Leila Badawi, “Islam”, in Jean Holm and John Bowker, ed., Women in Religion (London: Pinter Publishers, 1994) p.102.
[32] Amir H. Siddiqi, Studies in Islamic History (Karachi: Jamiyatul Falah Publications, 3rd edition, 1967) p. 102.

# SEHEMU 10

# TALAKA

Hizi dini tatu zina tofauti zilizo wazi kimtazamo juu ya talaka. Ukristo unapinga talaka moja kwa moja. Agano Jipya kwa kauli moja linapigania ndoa isiyotanguka. Inasemekana kuwa Yesu amesema: "*Lakini mimi nawaambia, kila mtu amwachaye mkewe, ispokuwa kwa habari ya uasherati, amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini*. (Matayo 5:32). Ukamilifu huo ulio mgumu kutekelezeka na usiobadilika bila ya shaka si jambo la hakika. Jambo hilo linaibua dhana ya ukamilifu wa kimaadili ambao haufikiwi na jamii ya kibinadamu. Wakati wanandoa wanapogundua kuwa ndoa yao haiwezi kuendelea, tendo la kuharamisha talaka haliwatendei wema wowote wanandoa hao. Kuwalazimisha wanandoa wanaochukiana waishio kwa ubaya wakae pamoja kinyume na matakwa yao ni jambo lisilo na maana yeyote wala si la haki. Si ajabu ulimwengu wa Wakristo wote unalazimisha kuruhusiwa kwa talaka.

Wayahudi, kwa upande mwingine, wanaruhusu talaka hata ikiwa bila sababu. Agano la kale linampa mume haki ya kumtaliki mkewe hata kama hana kosa au kwa kuwa hampendi tu.

“*Mtu akiisha kutwaa mke kwa kumwoa, asipopata kibali machoni mwake, kwa kuwa ameona neno ovu kwake, na amwandikie hati ya kumwacha, akamtilie mkononi mwake na kumtoa katika nyumba yake. Naye akiisha kuondoka katika nyumba yake, ana ruhusa kwenda akawa mke wa mtu mwingine. Na huyo mumewe wa sasa akimchukia, na kumwandikia hati ya kumwacha, na kumpa mkononi mwake, na kumtoa katika nyumba yake; au akifa yeye mumewe wa sasa, aliyemtwaa kuwa mkewe; yule wa kwanza aliyemwacha asimtwae kuwa mkewe tena, akiisha kutiwa unajisi; kwa kuwa haya ni machukizo mbele za BWANA; kwa hiyo asiitie dhambini nchi, akupayo BWANA, Mungu wako, iwe urithi.*” (Kum 24:1-4)

Aya iliyo hapo juu imesababisha mjadala mkali kwa Wanazuoni wa Kiyahudi kwa sababu ya kutokubaliana kwao juu ya tafsiri ya maneno. “Uovu, chuki, kutia aibu, tabia mbaya” na “kutopenda” yaliyotajwa katika hizo aya. Kitabu cha Talmudi kinasajili rai zao zilizotofauti tofauti:

“*Madhehebu ya Shamai inakamata kuwa mwanamume haruhusiwi kumwacha mkewe ila kama atampata na hatia ya uzinifu, huku madhehebu ya Hillel yanasema kuwa mwanamume anaweza kumwacha mkewe hata kama huyo mwanamke amevunja kibakuli cha mumewe. Na mwanazuoni Akiba anasema mwanamume anaweza kumwacha mke hata kama kwa sababu nyepesi ya kwamba amempata mwanamke mwingine aliyemzuri sana kuliko wa kwanza.*” (Gittin 90a-b).

Agano Jipya linafuata rai ya Shamaites huku sheria ya Kiyahudi imefuata rai ya Hillelites na R. Akiba[33] Tangu kuenea kwa rai ya Hillelites, imekuwa ni mafundisho yasiyokeukwa kwa sheria ya Wayahudi ya kuwapa uhuru wanaume wa kumuacha mkewe bila ya sababu yoyote. Agano la Kale sio tu linampa mume haki ya kumtaliki mkewe "*aliyemuhuzunisha*" lakini pia linazingatia kumwacha "*mke muovu*" ni lazima:

"*Mke mbaya analeta fedheha, muono wa kuhuzunisha, na maumivu ya moyo. Mgoigoi wa mkono na mdhaifu wa goti ni mwanamume ambaye mkewe ameshindwa kumfurahisha. Mwanamke ni dhambi ya asili, na kupitia kwake sote tutakufa. Usiache tangi lenye ufa kuchimba au kumruhusu mke mbaya asema atakacho. Na kama mwanamke huyo hakubali utawala wake, mwache na mfukuze*." (Ecclesiasticus 25:25).

Talmudi imesajili matendo maalumu kadhaa ya wake wanaolazimika kuachwa na waume zao: "*Kama mwanamke atakula mitaani, kama atakunywa kwa pupa mitaani, kama atanyonyesha mtaani, kwa matendo hayo yote mwanazuoni Meir amesema kuwa mwanamke huyo lazima aachane na mumewe*." (Git. 89a).

Vile vile Talmudi imefanya jambo hilo kuwa ni mamlaka ya kumuacha mwanamke mgumba (ambaye hazai kwa kipindi

[33] Epstein, op. cit., p. 196.

cha miaka kumi): "*Mwanazuoni wetu ametufundisha: Kama mwanamume amejitwalia mke na kuishi nae kwa miaka kumi na mwanamke huyo hajazaa mtoto, mwanamume huyo amuache mke huyo*." (Yeb. 64a).

Wake, kwa upande mwingine, hawawezi kutoa talaka chini ya ya sheria ya Kiyahudi. Mke wa Kiyahudi, hata hivyo, anaweza kuomba talaka mbele ya mahakama ya Kiyahudi huku akithibitisha sababu nzito ya kufanya hivyo. Ni nafasi ndogo sana apewayo mke ili aweze kuomba talaka. Miongoni mwa nafasi hizo ni: ikiwa mumewe ana ugonjwa mbaya au ugonjwa wa ngozi, mumewe akishindwa kutekeleza wajibu wa ndoa n.k. Hiyo mahakama inaweza kuunga mkono madai ya mke ya kutaka talaka lakini haina uwezo wa kuvunja ndoa. Ni mume tu awezaye kuvunja ndoa kwa kumtoza mkewe faini ya talaka. Na mahakama inao uwezo wa kutoa adhabu ya viboko, faini, kifungo na kumtenga na sinagogi huyo mume ili kumlazimisha apokee malipo ya lazima ya kumtaliki mkewe. Hata hivyo, kama mume atakuwa mbishi vya kutosha, anao uwezo wa kutotoa talaka na kuendelea kubaki na mkewe bila ya mipaka. Na baya zaidi, ni kuwa, mume anao uwezo wa kumtelekeza mkewe bila ya kumpa talaka na kumuacha akiwa si mwolewa wala si mtalikiwa. Na huyo mume anaweza kuoa mke mwingine au hata kuishi na kimada bila ya ndoa na kupata watoto kwa huyo kimada, (watoto hao wanahesabiwa kuwa ni wa halali katika sheria za Kiyahudi).

Mke aliyetelekezwa, kwa upande mwingine, haruhusiwi kuolewa na Myahudi mwingine, kwa kuwa yeye ni mke wa mtu kisheria na hawezi kuishi na mwanamume mwingine kwa sababu atahesabiwa kuwa ni mzinifu na watoto wake kwa huyo mwanamume mwingine pia si wa halali kwa vizazi kumi. Mwanamke atakayekuwa katika hali hiyo anaitwa agunah (yaani mwanamke aliyetundikwa).[34] Leo hii nchini Marekani kuna, takriban maagunot 1000 hadi 1500 miongo mwa wanawake wa Kiyahudi ambao ni maagunoti (agunot ni wingi wa agunah), wakati nchini Israeli idadi yao ni kubwa kufikia kiasi cha 16,000. Waume wanaweza kunyang`anya maelfu ya dola kutoka kwa wake zao waliowatia mtegoni na hiyo ikiwa ni malipo ya talaka ya Kiyahudi.[35]

Uislamu unashikilia nafasi ya katikati baina ya Ukristo na Uyahudi, pamoja na kuiheshimu talaka. Ndoa katika Uislamu ni kufunga mkataba mtakatifu ambao hauruhusiwi kuvunjwa ila kwa sababu nzito. Wanandoa wanafundishwa watafute kila njia ya kutatua matatizo yao ili waokoe ndoa yao, iliyo hatarini.

Talaka isiwe ndio kimbilio ila kama kutakuwa hukana njia nyingine ispokuwa talaka. Kwa ufupi, Uislamu unaikubali talaka, hata hivyo hauipendi hata kidogo. Hebu kwanza

[34] Swidler, op. cit., pp. 162-163.
[35] The Toronto Star, Apr. 8, 1995.

tuangalie upande wa kuitambua. Uislamu unatambua haki ya wanandoa ya kumaliza uhusiano wao wa kindoa.

Uislamu unampa mume haki ya kutoa (talaka). Zaidi ya hayo, Uislamu ni kinyume na Uyahudi, unampa mke haki ya kuvunja ndoa kupitia kile kijulikanacho kama khulah.[36] Kama mume atavunja ndoa kwa kumtaliki mkewe, hatorudishiwa chochote miongoni mwa mahari aliyotoa kumpa mkewe. Quran imeeleza kuharamisha kwa mume aliyeacha mke asirudishiwe mahari bila kujali ughali au thamani ya mahari yenyewe:

*"Na kama mkitaka kubadilisha mke mahali pa mke, (yaani kumwoa mke mwingine na kumwacha huyo wa zamani), na hali mmoja wao (nae ndiye huyo anayemwacha) mumempa mrundi wa mali, basi msichukue chochote. Je, mnachukua kwa dhulma na kwa khatia iliyo wazi?" (Quran 4:20)*

Katika hali ya mke kuamua kumaliza ndoa, huyo mke anatakiwa arejeshe mahari kwa mumewe. Kurejesha mahari katika hali hii ni fidia ya uadilifu kwa mume ambaye anapendelea kuendelea na mkewe huku huyo mke anataka waachane.

[36] Sabiq, op. cit., pp. 318-329. See also Muhammad al Ghazali, Qadaya al Mar`aa bin al Taqaleed al Rakida wal Wafida (Cairo: Dar al Shrooq, 4th edition, 1992) pp. 178-180.

Quran imewafundisha waume wa Kiislamu wasichukue kitu chochote katika mahari walizowapa wake zao ispokuwa katika hali ya mke kuamua kuvunja ndoa:

"…*Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa (wake zenu), ispokuwa (wote wawili) wakiogopa ya kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu. Basi mkiogopa kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu, hapo itakuwa hapana dhambi kwao (mwanaume wala mwanamke katika) kupokea (au kutoa) ajikomboleacho mwanamke. Hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu; basi msiiruke. Na watakaoiruka mipaka Mwenyezi Mungu, hao ndio madhalimu (wa nafsi zao)*. (Quran 2:229)

Pia, mwanamke mmoja alimuendea Mtume Muhammad (S.A.W) akitaka kuvunjwa kwa ndoa yake, akamwambia Mtume kwamba yeye hana lalamiko lolote dhidi ya tabia au hali ya mumewe. Tatizo lake la pekee lilikuwa ni kuwa hampendi huyo mume, na hawezi kuendelea kuishi naye. Mtume (S.A.W) akamuuliza: "*Je, utamrudishia bustani yake? (mahari aliyokupa) Akasema: "Ndio" Kisha Mtume (S.A.W) akamfundisha yule mwanamume apokee bustani yake na akubali kuvunjika kwa ndoa*. (Bukhari)

Katika baadhi ya hali, mke wa Kiislamu huenda akawa anataka kuendelea na ndoa lakini anajikuta analazimika adai talaka kwa sababu kuna sababu zinazolazimisha kufanya hivyo kwa mfano: ukatili wa mume, kutelekezwa bila sababu,

mume kushindwa kutimiza majukumu yake ya ndoa n.k. Katika hali hizi mahakama ya Kiislamu inavunja ndoa.[37]

Kwa muhtasari, Uislamu umempa mwanamke wa Kiislamu baadhi ya haki zisizo na kifani; mwanamke anaweza kumaliza ndoa kupitia khulah na kufungua mashitaka ya kudai talaka. Mke wa Kiislamu kamwe hatokuwa mtundikwa na mume mkaidi. Na zilikuwa ni haki hizi zilizowashawishi wanawake wa Kiyahudi waliokuwa wakiishi katika jamii za Kiislamu za mwanzo za karne ya saba C.E. watafute kupata malipo ya talaka kutoka kwa waume zao wa Kiyahudi kupitia mahakama za Kiislamu. Wanazuoni wa Kiyahudi walitangaza kuwa malipo hayo ni batili na hayafai. Ili kukomesha mwenendo huo, wanazuoni wa Kiyahudi walitoa haki mpya na marupurupu kwa wanawake wa Kiyahudi ili kujaribu kudhoofisha mvuto wa mahakama za Kiislamu. Wanawake wa Kiyahudi waishio katika nchi za Kikristo hawakupewa chochote katika marupurupu kama yale ya wenzao. Kwa kuwa sheria ya talaka ya Kirumi inayofanyakazi ilikuwa haina mvuto wa ziada kuliko sheria za Kiyahudi.[38]

Sasa, hebu acha tutazame namna Uislamu usivyopendelea talaka. Mtume wa Uislamu amewaambia waumini kuwa:

[37] Ibid., pp. 313-318.
[38] David W. Amram, The Jewish Law of Divorce According to Bible and Talmud (Philadelphia: Edward Stern & Con., Inc., 1896) pp. 125-126.

"*Jambo la halali linalomchukiza sana Mwenyezi Mungu ni talaka*." (Abu Dawood).

Mwanamume wa Kiislamu hatakiwi kumtaliki mkewe eti kwa kuwa hampendi. Quran inawafundisha wanaume wa Kiislamu wawe wema kwa wake zao hata katika hali ya hisia za kuvuvuwaa au hisia za kutompenda:

"*….Na kaeni nao kwa wema; na kama mkiwachukia basi (msiwaache) kwani huenda mkakichukia kitu, na Mwenyezi Mungu ametia kheri nyingi ndani yake*. (Quran 4:19)

Mtume Muhammad (S.A.W) ametoa mafundisho kama hayo:

"*Muumini wa kiume asimchukie muumini wa kike, kama hapendi moja ya tabia zake atapendezwa na nyinginezo*." (Muslim).

Vile vile, Mtume, amesisitiza kuwa Waislamu wabora sana ni wale walio wabora kwa wake zao:

"*Mkamilifu wa imani miongoni mwa waumini ni yule mbora wao kitabia, na aliye mbora wenu kitabia ni yule mwenye tabia njema kwa mkewe."* (Tirmidhi)

Hata hivyo, Uislamu ni dini ya vitendo na inatambua kuwa kuna wakati ndoa inakuwa ipo ukingoni karibu kuvunjika. Katika hali kama hizo, ushauri mtupu wa kuwa mwema au kujizuia nafsi, unakuwa hauna utatuzi wa kutosheleza. Kwa hiyo, nini cha kufanya ili kuokoa ndoa katika hali ngumu

kama hizo? Quran inatoa baadhi ya ushauri wa kutendwa kwa wanandoa (mume au mke) ambaye mwenziwe (mke au mume) ni muovu. Kwa mume ambaye mkewe ana tabia mbaya inayotishia ndoa, Quran inatoa aina nne za ushauri kama zilivyoelezwa kikamilifu katika aya zifuatazo:

"*…Na wanawake ambao mnaona uasi wao kwenu; (1) waonyeni (2) na waacheni peke yao katika vitanda (3) na wapigeni. Na kama wanakutiini msiwatafutie njia (ya kuwaudhi bure). Hakika Mwenyezi Mungu ndiye aliye juu (na) Mkuu. (4) Na kama mkijua kuwa kuna ugomvi baina ya mke na mume basi pelekeni mwamuzi mmoja katika jamaa za mwanamume na mmoja katika jamaa za mwanamke. Kama wakitaka mapatano Mwenyezi Mungu atawawezesha. Hakika Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa habari za siri na habari za dhahiri*. (Quran 4:34-35)

Mambo matatu ya kwanza kutajwa yajaribiwe kwanza. Na kama yameshindwa, ndipo inapotakiwa kutafutwa msaada wa familia. Ni lazima izingatiwe, kuwa aya za hapo juu zinaangaza, kuwa kumpiga mke mkaidi, ni kipimo cha muda mfupi ambacho kinakimbiliwa kikiwa ni hatua ya tatu tena katika hali ya kulazimika kufanya hivyo huku kukiwa na matarajio ya kuwa hiyo itakuwa dawa ya matendo maovu ya mke. Kama hilo litafaa, basi mume haruhusiwi kwa hali yoyote ile kuendelea kumsumbua mke kama ilivyotajwa kwa ufafanuzi katika aya hizo. Na kama njia hiyo imeshindwa, mume bado haruhusiwi kutumia tena njia hiyo na hapo ndipo

njia ya mwisho ya suluhisho kwa msaada wa familia lazima iangaliwe.

Mtume Muhammad (S.A.W) amewafundisha waumini wa Kiislamu ya kuwa wasitumie njia hiyo ila katika hali ya mwisho kabisa kama vile uasherati wa wazi uliotendwa na mke. Hata katika hali kama hiyo adhabu inatakiwa iwe nyepesi na kama mke ataacha, mume haruhusiwi kumsumbua tena:

"*Kama watafanya uasherati wa wazi wahameni vitandani, na wapigeni mapigo hafifu. Na kama watakutiini, msiwatafutie sababu ya kuwasumbua*." (Tirmidhi).

Kwa kuongezea, Mtume wa Uislamu amelaani mapigo yoyote yasiyo ya kiuadilifu. Baadhi ya wake wa Kiislamu walimshitakia Mtume (S.A.W) kuwa waume zao wamewapiga. Kwa kusikia hivyo, Mtume kwa dhahiri alisema kuwa:

"*Wale wafanyao hayo (kuwapiga wake zao) si wabora wenu*." (Abu Dawood).

Lazima ikumbukwe kuwa katika nukta hii Mtume pia amesema:

"*Mbora wenu ni yule mbora kwa familia yake, nami ni mbora wenu kwa familia yangu*." (Tirmidhi).

Mtume (S.A.W) alimshauri mwanamke mmoja wa Kiislamu, jina lake lilikuwa ni Fatuma binti Qaisi, asiolewe na jamaa mmoja kwa sababu jamaa huyo alikuwa anajulikana kwa kuwapiga wanawake.

"*Nilimwendea Mtume na kumwambia: Abul Jahm na Mu'awiah wanataka kunioa. Mtume Muhammad (S.A.W) (kwa njia ya ushauri) alisema: Mu'awiah ni masikini sana na Abul Jahm amezoea kuwapiga wanawake.*" (Muslim).

Lazima ifahamike kuwa ruhusa ya Talmudi ya kumpiga mke kwa kumuadabisha kwa lengo la kumnyoosha.[39] Mume hajawekewa mipaka kwa kesi kubwa kubwa kama za uasherati wa wazi. Ameruhusiwa kumpiga mkewe hata kwa kukataa kufanya kazi za nyumbani. Zaidi ya hayo, mume hajawekewa mipaka ya kutumia haki ya kuadhibu. Ameruhusiwa kuvunja ushupavu wa mkewe kwa mjeledi au kwa kumshindisha na njaa.[40]

Kwa mke ambaye mumewe ana tabia mbaya inayosababisha ndoa ikaribie kuvunjika, Quran inatoa ushauri ufutao:

"*Na kama mke akiona kwa mume wake kugombanagombana na kutenganatengana, basi si vibaya kwao wakitengeneza baina yao sulhu (njema wakastahmiliana vivyo hivyo bila kuachana); maana sulhu ni kitu bora. Na nafsi zimewekewa*

[39] Epstein, op. cit., p. 219.
[40] Ibid, pp 156-157.

*ubakhili mbele (ya macho yake). Na kama mkifanya mema (kuwafanyia wake zenu hao msiowapenda) na mkimcha Mwenyezi Mungu (msiwapunguzie haki zao, basi bila ya shaka Mwenyezi Mungu atakulipeni), kwani Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayoyatenda*. (Quran 4:128).

Katika hali hii, mke ameshauriwa atafute suluhu na mumewe (akiwa na msaada wa familia au bila familia). Ni jambo linalofahamika kuwa Quran si yenye kumshauri mke akimbilie njia mbili za kugomea ngono na kupiga. Na sababu ya tofauti hii ni kumkinga mke na majibu makali mno ya kuumiza mwili kutoka kwa mumewe ambaye tayari ashakuwa na tabia mbaya. Majibu hayo yanaweza kusababisha kuathirika kwa wote wawili mke na mume pamoja na ndoa na kuleta hali mbaya kuliko kuleta hali nzuri. Baadhi ya wanazuoni wa Kiislamu wamependekeza kuwa mahakama inaweza ikatekeleza njia hizo dhidi ya mume kwa niaba ya mke. Hiyo ni kuwa, kwanza mahakama imuonye mume aliyekengeuka, kisha imkataze kitanda cha mkewe, na mwisho itekeleze kipigo cha aina yake. [41]

Kwa kumalizia, Uislamu unawapa waliooana ushauri mwingi unaowezekana ili kuokoa ndoa zao wakati wa matatizo na migogoro. Na kama mmoja wa wanandoa anahatarisha mafungamano ya mambo ya ndoa, mwanandoa mwenza ameshauriwa na Quran afanye kila kiwezekanacho na chenye

[41] Muhammad Abu Zahra, Usbu al Fiqh al Islami (Cairo: al Majlis al A`la li Ri`ayat al Funun, 1963) p.66.

kuleta manufaa ili aokoe huo muungano mtakatifu. Na kama njia zote zimeshindwa, Uislamu unaruhusu wanandoa waachane kwa amani na kwa wema.

# SEHEMU 11

# AKINA MAMA

Agano la Kale katika sehemu nyingi linaamrisha wema na kutenda matendo ya pekee kwa wazazi na kuwalaani wale ambao hawawatendei wema. Kwa mfano, "*Kwa maana kila mtu amlaaniye baba yake au mama yake hakika atauawa; amemlaani baba yake na mama yake; damu yake itakuwa juu yake*." (Mambo ya walawi 20:9) na "*Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye; bali mpumbavu humdharau mamaye*." (Mithali 15:20).

Ingawa kumfanyia wema baba peke yake ndiko kulikotajwa katika baadhi ya sehemu; kwa mfano, "*Mwana mwenye hekima husikiliza mausia ya babaye; Bali mwenye dharau hasikilizi maonyo."* (Mithali 13:1) Mama peke yake ndiye asiyetajwa. Zaidi ya hayo, hakuna msisitizo wa kipekee juu ya kumtendea wema mama kama alama ya kufahamu vizuri tabu nyingi alizozipata wakati wa kujifungua na matatizo ya mtoto mchanga. Kando ya hayo, akina mama hawarithi

kabisa kabisa chochote toka kwa watoto wao huku akina baba wanarithi.[42]

Ni vigumu kusema kuwa Agano Jipya ni maandiko yanayowataka watu wawafanyie wema akinamama. Kwa kulinganisha, mtu anaona kuwa Agano Jipya linahesabu kuwatendea wema akinamama kuwa ni kikwazo katika njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa mujibu wa Agano Jipya, mtu hawezi kuwa Mkristo mzuri wa kutumainiwa kuwa yeye ni mfuasi wa Kristo ila amchukie mama yake. Inasemekana kuwa Yesu alisema:

"*Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake; naam na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu."* (Luka 14:26)

Kwa kuongezea, Agano Jipya linatoa picha ya Yesu kama ni mtu mwenye tofauti au asiyemuheshimu mama yake mzazi. Kwa mfano, wakati mama yake alipokwenda kumtafuta na huku Yesu akiwa anawahubiria makutano, Yesu hakujali wala hakutoka kwenda kumuona mama yake:

"*Wakaja mamaye na nduguze; wakasimama nje, wakatuma mtu kumwita. Na makutano walikuwa wameketi, wakimzunguka; wakamwambia, Tazama, mama yako na ndugu zako wako nje, wanakutafuta. Akawajibu, akisema,*

[42] Epstein, op. cit., p. 122.

*Mama yangu na ndugu zangu ni akina nani? Akawatazama wale walioketi wakimzunguka pande zote, akasema, Tazama, mama yangu na ndugu zangu! Kwa maana mtu ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu."* (Marko 3:31-35).

Mtu anaweza akadai kuwa Yesu alikuwa akijaribu kuwafundisha makutano yake somo muhimu sana ambalo ni kuwa uhusiano wa kidini si wenye umuhimu mdogo kuliko uhusiano wa kifamilia. Hata hivyo, Yesu alikuwa na uwezo wa kuwafundisha wasikilizaji wake somo hilo hilo bila ya kuonyesha huko kutomjali mama yake kulikokuwa kwa wazi wazi. Mwelekeo kama huo usio na heshima unatoa picha ya wakati alipokataa kuthibitisha maelezo yaliyotolewa na makutano yake ya kuibariki kazi ya mama yake ya kumzaa na kumlea:

"*Ikawa alipokisema maneno hayo, mwanamke mmoja katika mkutano alipaza sauti yake, akamwambia, Heri tumbo lililokuzaa, na matiti uliyonyonya. Lakini yeye alisem, Afadhali, heri walisikiao neno la Mungu na kulishika."* (Luka 11:27-28)

Ikiwa mama mwenye daraja ya bikira Maria ametendewa matendo yasio na heshima kiasi hicho, kama ilivyofafanuliwa na Agano Jipya, tena katendewa na mtoto mwenye daraja ya Yesu Kristo, sasa itakuwaje kwa mama wa kawaida wa Kikristo vipi atatendewa na wanawe wa Kikristo wa kawaida?

Katika Uislamu, heshima, utiifu, na kutukuza kunaambatana na mfano ambao hauna kifani. Quran inaweka umuhimu wa kuwatendea wema wazazi kuwa ni jambo la pili baada ya kumuabudu Mwenyezi Mungu Muweza:

*"Na Mola wako amehukumu kuwa msimuabudu yoyote ila Yeye tu. Na (ameagiza) kuwafanyia wema (mkubwa) wazazi. Kama mmoja wao akifikia uzee, (naye yuko) pamoja nawe, au wote wawili, basi usiwaambie hata Ah! Wala usiwakemee. Na useme nao kwa msemo wa hishima (kabisa). Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa (njia ya kuwaonea) huruma (kwa kuwaona wamekuwa wazee). Na useme; "Mola wangu! Warehemu (wazee wangu) kama walivyonilea katika utoto."* (Quran 17:23-24)

Quran katika sehemu kadhaa imeweka mkazo maalumu kwa kazi ya mama ya kuzaa na kulea:

*"Na tumemuusia mwanadamu (kuwafanyia ihsani) wazazi wake – mama yake ameichukuwa mimba yake kwa udhaifu juu ya udhaifu, na (kumnyonyesha na kuja) kumwachisha kunyonya katika miaka miwili – ya kwamba unishukuru mimi na wazazi wako; marejeo yenu ni kwangu,"* (Quran 31:14)

Nafasi ya pekee ya akina mama katika Uislamu imeelezwa kwa umbuji (ufundi wa kupanga na kutumia maneno kwa ujuzi wa hali ya juu sana) na Mtume Muhammad (S.A.W):

*"Mtu mmoja alimuuliza Mtume: "Ni nani nimfanyie wema zaidi? Mtume (S.A.W) akamjibu: "Mama yako". "Na nani*

*anafuata?" Aliuliza yule jamaa. Mtume (S.A.W) akamjibu: "Mama yako". "Na nani anafuata?" Aliuliza yule jamaa Mtume (S.A.W) akamjibu: "Mama yako". "Na nani anafuata?" Aliuliza yule jamaa. Mtume (S.A.W) akamjibu: "Baba yako".* (Bukhari na Muslim).

Miongoni mwa mafundisho machache ya Uislamu ambayo kwa imani kabisa Waislamu wanayachunga hadi leo hii ni kuwatendea wema akina mama. Heshima wanayoipata akina mama wa Kiiaslamu kutoka kwa watoto wao wa kiume na wa kike inaonyeshwa kwa mifano. Nguvu kali na mafungamano motomoto baina ya akinamama wa Kiislamu na watoto wao na heshima ya kina ambayo wanaume wa Kiislamu wanawafanyia mama zao kwa kuwasaidia inawashangaza watu wa Magharibi.[43]

[43] Armstrong, op. cit., p, 8.

# SEHEMU 12

# MIRATHI KWA WANAWAKE.

Moja ya tofauti kubwa kati ya Quran na Biblia ni mitazamo yao juu ya mirathi ya wanawake kurithi mali za ndugu zao waliofariki. Mtazamo wa Kibiblia una maneno mafupi yaliyowazi na yalioelezwa na mwanazuoni Epstein: "*Mafundisho yanayoendelea na yasiyovunjika tangu enzi za kuanza Biblia hayampi mwanamke, mke na mabinti haki ya kurithi mali ya familia. Katika mfumo mkongwe sana wa urithi, wanafamilia wa kike wanazingatiwa kuwa ni sehemu ya mali ya urithi na kuwa ni watu wa mbali kabisa na utu, kisheria wanarithiwa na kuwa wao ni kama watumwa. Wakati ambapo kanuni za Musa zinatoa mirathi kwa mabinti ikiwa hakuna mwanaumume. Lakini hata hivyo mke harithi hata katika hali kama hiyo.*[44] Kwa nini wanafamilia wa kike wanachukuliwa kuwa ni sehemu ya urathi? Mwanazuoni Esptein ana jibu: *"Wanawake ni miliki ya baba zao kabla ya kuolewa na ni miliki ya waume zao baada ya kuolewa.*"[45]

---

[44] Epstein, op. cit., p. 175.
[45] Ibid., p. 121.

Sheria za mirathi za Biblia zimeelezwa katika Hesabu 27:1-11. Mke hapewi fungu lolote katika mirathi ya mumewe, huku huyo mume ndio mrithi wa kwanza wa kumrithi mkewe, tena hata kabla ya watoto wake. Binti anaweza kurithi kama tu hakuna mwanamume wa kurithi. Mama harithi kabisa kabisa huku baba akirithi. Wajane na mabinti, katika hali ya kuwepo watoto wa kiume, wamo katika huruma ya warithi wa kiume kwa kusaidiwa. Na hiyo ndiyo sababu wajane na mayatima wa kike wamekuwa ni miongoni mwa mafukara sana katika jamii ya Kiyahudi.

Ukristo umekuwa ukifuata sheria hizo hizo kwa muda mrefu. Sheria zote mbili za kikanisa na za kiraia kwa Wakristo zinazuia mabinti wasishirikiane na kaka zao katika urithi kutoka kwa baba yao. Kando ya hayo, wake walikuwa wananyimwa haki zote za kurithi. Sheria hiyo ya udhalimu sana ilidumu hadi mwishoni mwa karne iliyopita.[46]

Miongoni mwa wapagani wa Kiarabu kabla ya Uislamu, haki za kurithi zilikuwa kwa ndugu wa kiume tu. Quran imekomesha dhuluma zote hizo za kiutamaduni na ukawapa ndugu wote wa kike mafungu ya kurithi:

"*Wanaume wana sehemu katika mali wanayoyaacha wazazi na jamaa waliokaribia. Na wanawake (pia) wanayo sehemu katika yale waliyoyaacha wazazi na jamaa waliokaribia.*

[46] Gage, op. cit., p. 142.

*Yakiwa kidogo au mengi. (Hizi) ni sehemu zilizofaridhiwa (na Mwenyezi Mungu)*. (Quran 4:7)

Akina mama, wake, wasichana na madada wa Kiislamu wamepokea haki za kurithi miaka elfu moja na mia tatu kabla ya Ulaya kutambua kuwepo kwa haki hiyo. Mgawo wa urithi ni somo kubwa sana lenye maelezo kamili katika (Quran 4:7, 11, 12, 176). Sheria mama ni kuwa fungu la mwanamke ni sawa sawa na nusu ya mwanamume ispokuwa katika hali ambazo mama anapata sawa sawa na baba. Hii sheria mama kama itachukuliwa kwa kutengwa kutoka katika sheria nyinginezo zinazowahusu wanaume na wanawake inawezekana kuonekana kuwa haina uadilifu. Ili kufahamu uwiano uliopo katika sheria hii, mtu lazima azingatie ukweli kwamba mujukumu ya kipesa kwa wanaume katika Uislamu yanazidi sana yale ya wanawake (Tazama kitengo cha *mali za wanawake*). Mume lazima ampe mkewe mahari. Mahari hiyo ni mali ya huyo mke na inaendelea kuwa hivyo hivyo hata kama ataachwa hapo baadaye.

Bi harusi hana wajibu wa kutoa kitu cha kumpa bwana harusi. Zaidi ya hayo, mume wa Kiislamu anachajiwa huduma za mkewe na wanawe. Mke, kwa upande mwingine, halazimishwi kumsaidia mumewe katika majukumu haya. Mali na pato la mke ni kwa ajili yake binafsi ila kile atakachojitolea kumpa mumewe. Kando ya hayo, mtu lazima atambue kuwa Uislamu kwa juhudi kubwa unahimiza maisha ya kifamilia. Uislamu kwa nguvu sana unawahimiza vijana waoane, na unahimiza kutoachana na haupendi useja (utawa,

hali ya kutooa au kutoolewa) eti jambo hilo ni maadili mema. Kwa hiyo, katika jamii sahihi ya Kiislamu, maisha ya kifamilia (ndoa) ndio kitu cha kawaida na maisha ya kutooa au kutoolewa ni mara chache sana kuwepo. Hiyo ni kwa kuwa, takriban wanawake wote walio katika umri wa kuolewa na wanaume waliofikia umri wa kuoa wameoana katika jamii za Kiislamu. Katika mwanga wa uhakika huu, mtu anaweza kufahamu vizuri kuwa wanaume wa Kiislamu, kiujumla, wana mzigo mkubwa sana wa kiuchumi kuliko wanawake kwa hiyo sheria za mirathi zinamaanisha kufidia kutowiana huko kiasi ambacho jamii nzima itaishi bila ya kuwa na vita vyovyote vya kijinsia au kitabaka. Baada ya mlinganisho mdogo kati ya haki za kiuchumi na wajibu wa wanawake wa Kiislamu, mwanamke mmoja wa Kiislamu ambaye ni Mwingereza, amehitimisha kuwa Uislamu unawatendea wanawake sio tu kiuadilifu lakini pia unawatendea vizuri zaidi.[47]

[47] B.Aisha Lemu and Fatima Heeren, Woman in Islam (London: Islamic Foundation, 1978) p.23.

# SEHEMU 13

# HALI MBAYA YA WAJANE

Kwa sababu ya ukweli kwamba Agano la Kale halitambui haki yoyote kwa wanawake, wajane wamekuwa ni miongoni mwa watu masikini sana katika jamii ya Kiyahudi. Ndugu wa kiume ambao wamerithi mali yote ya mume aliyefariki ambayo ilikuwa apewe huyo mke kutoka katika mali hiyo. Hata hivyo, wajane hawana jinsi ya kujihakikishia matumizi hayo ambayo yameshasombwa, na wanaishi kwa kungojea huruma za watu wengine. Kwa hiyo wajane wamekuwa ni watu wa daraja la chini mno katika Israeli ya zamani na ujane ulizingatiwa kuwa ni alama ya kushuka hadhi sana (Isaya 54:4). Lakini hali mbaya ya mjane katika mafundisho ya Kibiblia inaenea hadi nga`mbo ya kutengwa kutoka katika mali ya mumewe. Kwa mujibu wa Mwanzo 38, mjane asiye na mtoto lazima aolewe na ndugu wa mumewe, hata kama atakuwa ameshaoa, kwa hiyo huyo ndugu azae mtoto kwa ajili ya kaka yake aliyefariki, jambo ambalo litaimarisha jina la ndugu yake na halitokufa.

"*Yuda akamwambia Onani, uingie kwa mke wa nduguyo ukamwoe, ukamwinulie nduguyo uzao.*" (Mwanzo 38:8).

Radhi za mjane kuridhia ndoa hiyo hazihitajiki. Mjane anatendewa kama ni sehemu ya mali ya mumewe aliyefariki, mke ambaye faida yake kuu ni kuhakikisha kizazi cha mumewe. Hii sheria ya Kibiblia bado inatumiwa katika Israeli ya leo.[48] Mjane asiye na mtoto katika Israeli ni ridhisho la ndugu wa mumewe. Na kama huyo ndugu ni mdogo sana hata hawezi kuoa, mjane huyo lazima amsubiri hadi afikie umri wa kuoa. Kama huyo ndugu akikataa kumuoa, atakuwa huru na anaweza kuolewa na mtu yeyote aliye chaguo lake. Hilo ni tukio lisilo la kawaida nchini Israeli kwani wajane ni watu wa kukandamizwa na shemeji zao ili wapate uhuru wao.

Wapagani wa Kiarabu kabla ya Uislamu walikuwa na matendo hayo hayo. Mjane alikuwa akichukuliwa kuwa ni sehemu ya mali ya mume na anarithiwa na warithi wake wa kiume na huyo mke alikuwa, mara nyingi, akitolewa aolewe na mtoto mkubwa wa mumewe aliezaliwa na mke mwingine. Quran kwa ukali imeshambulia na kutokomeza mila hii ya kudhalilisha:

"*Wala msiwaoe wake waliowaoa baba zenu; ispokuwa yale yaliokwisha pita. (Yaliyopita yamepita yasirejeshwe tena). Bila ya shaka jambo hili ni uovu na uchukizo na ni njia mbaya." (Quran* 4:22)

[48] Hazleton, op.cit., pp. 45-46.

Wajane na wanwake walioachwa wanadhalilishwa sana katika itikadi ya Kiyahudi kiasi ambacho Kuhani Mkuu hakuruhusiwa kumuoa mjane, mtalikiwa, au malaya:

"*Naye atamwoa mwanamke katika ubikira wake. Asitwae mjane, wala mwanamke aliyeachwa na mumewe, wala mwanamke mwenye unajisi, wala kahaba; lakini atamwoa mwanamwali katika watu wake mwenyewe. Naye asiwatie unajisi kizazi chake katika watu wake; kwa kuwa mimi ndimi BWANA nimtakasaye.*" (Walawi 21: 13-15)

Leo hii katika Israeli, mjukuu mwenye hadhi ya Cohen (Kuhani Mkuu wa siku za hekaluni) haruhusiwi kumuoa mtalikiwa, mjane au kahaba.[49] Katika sheria za Kiyahudi, mwanamke aliyewahi kuwa mjane kwa mara tatu ikiwa wanaume wote watatu wamekufa kwa sababu za kikawaida mwanamke huyo anahesabiwa kuwa ni janga na ni haramu kuolewa tena.[50] Quran kwa upande mwingine, haimchukulii mtu yeyote kuwa ni wa bahati wala ni wa mikosi. Wajane na watalikiwa wana uhuru wa kuolewa na mwanamume yeyote wamtakaye.

Hakuna aibu inayomkumba mtalikiwa au mjane katika Quran:

[49] Ibid., p.47.
[50] Ibid., p. 49.

*“Na mtakapowapa wanawake talaka, nao wakafikia kumaliza eda yao, basi warejeeni kwa wema au tokaneni nao kwa wema. Wala msiwaweke kwa kuwapa dhara mkaruka mipaka. Na atakayefanya hivyo, amejidhulumu mwenyewe. Wala msizifanyie mzaha Aya za Mwenyezi Mungu. Na mkumbuke neema za Mungu zilizo juu yenu, na (khasa ile neema ya) kuteremshiwa Quran; na (kujuvywa) ilimu nyingine anazokuonyeeni. Na mcheni Mwenyezi Mungu na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu.”* (Quran 2:231)

*“Na wale wanaofishwa (wanaokufa) miongoni mwenu na kuacha wake; hawa (wake) wangoje (wasiolewe) miezi minne na siku kumi. Na wanapofikia muda wao (wa kumaliza eda yao hiyo), basi si dhambi juu yenu kwa yale wanayoyafanyia nafsi zao (hao wanawake) kwa yanayowafiki (kufuata) Sharia. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za yote mnayoyatenda.* (Quran 2:234)

*“Na wale wanaofishwa (wanaokufa) miongoni mwenu na wakawaacha wake, wawausie (mawarithi wao) kwa ajili ya wake zao kupata matumizi kwa mwaka mmoja bila ya kutolewa (katika majumba waliyokuwamo, ya waume zao). Na kama wanawake (wenyewe) wakiondoka, basi si kosa juu yenu kwa yale waliyoyafanya kwa nafsi zao wenyewe yanayofuata Sharia. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.* (Quran 2:240)

# SEHEMU 14
# UKEWENZA

Kwa sasa acha tushughulikie suala muhimu la mitala. Mitala ni jambo la zamani sana linalopatikana katika jamii za kibinadamu nyingi. Biblia haijakemea mitala. Kwa kulinganisha, Agano la Kale na maandiko ya wanazuoni wa Kiyahudi mara kwa mara yanathibitisha haki ya mitala. Inasemekana kuwa mfalme Suleimani alikuwa na wake 700 na masuria 300. (1 Wafalme 11:3) Vile vile, mfalme Daudi, inasemekana alikuwa na wake wengi na masuria pia (2 Samweli 5:13). Agano la Kale lina sheria za kugawa mali za mume na kuwapa watoto wake kutoka kwa wake mbali mbali. (Kumb. 22:7). Kizuizi cha pekee dhidi ya mitala ni kuharamishwa kumtwaa dada wa mkeo awe mke mwenza. (Walawi 18:18). Talmudi inashauri idadi ya mwisho kuwa ni wake wanne.[51] Wayahudi wa Ulaya waliendelea kufanya mitala hadi karne ya kumi na sita. Mayahudi wa kimashariki kikawaida wanatekeleza mitala hadi walipofika Israeli, ambako kuliharamishwa mitala chini ya sheria ya uraia. Hata

[51] Swidler, op. cit., pp. 144-148.

hivyo, katika sheria za kidini ambazo zinapuuza sheria za kiraia katika shauri hilo, mitala imeruhusiwa.[52]

Je, Agano Jipya lina nini? Kwa mujibu wa Baba Eugene Hilman katika kitabu chake cha utambuzi, mitala inachukuliwa hivi: *"Hakuna sehemu yeyote katika Agano Jipya yenye amri iliyo wazi kuwa ndoa yatakiwa iwe ya mke mmoja au mume mmoja au amri yeyote inayoharamisha mitala*."[53] Zaidi ya hayo, Yesu hajasema kitu dhidi ya mitala ingawa ilikuwa ikifanywa na Wayahudi wa jamii yake. Baba Hilman ametilia mkazo uhakika wa kuwa Kanisa huko Roma liliharamisha mitala ili kufuata mila ya Kigiriki-Kirumi (ambayo imeamuru kuwa na mke mmoja tu wa kisheria huku ikiruhusu vimada na umalaya). Naye alimtaja Mt. Augustine, "*Sasa kwa hakika muda wetu huu, na kwa kuishi na mila za Kirumi, hairuhusiwi kujitwalia mke mwingine*."[54]

Makanisa ya Kiafrika na Wakristo wa Kiafrika mara nyingi wanawakumbusha wenziwao wa Ulaya kuwa Kanisa kuharamisha mitala ni mila za utamaduni na sio amri ya sheria thabiti ya Kikristo.

Quran, vile vile imeruhusu ukewenza, lakini sio bila ya mipaka:

---

[52] Hazleton, op. cit., pp 44-45.
[53] Eugene Hillman, Polygamy Reconsidered: African Plural Marriage and the Christian Churches (New York: Orbis Books, 1975) p. 140.
[54] Ibid., p. 17.

"*Na kama mkiogopa kutowafanyia uadilifu mayatima (basi ogopeni vile vile kutowafanyia uadilifu wanawake). Basi oeni mnaowapenda katika wanawake, (maadamu mtawafanyia insafu) wawili au watatu au wanne (tu). Na mkiogopa kuwa hamuwezi kufanya uadilifu, basi (oeni) mmoja tu, au (wawekeni masuria) wale ambao mikono yenu ya kiume imewamiliki. Kafanya hivi ndiko kutapelekea kutofanya jeuri*." (Quran 4:3)

Quran, kinyume na Biblia, imeweka mipaka ya idadi ya wake hadi wanne tena chini ya masharti makali ya kuwatendea hao wake kwa usawa na uadilifu. Isifahamike kuwa Quran inawahimiza waumini wafanye mitala, au kuwa na mitala ndio ukamilifu. Kwa maneno mengine, Qurani "*imesamehe*" au "*imeruhusu*" mitala, na si zaidi, lakini kwa nini? Kwa nini mitala imeruhusiwa? Jibu ni lepesi: kuna maeneo na nyakati ambazo zinalazimisha jamii kufanya hivyo, pia malengo ya kimaadili ya kuwepo kwa mitala. Kama aya ya Quran iliyopo hapo juu ilivyoonyesha, mada hii ya mitala katika Uislamu haitofahamika peke yake nje ya shuruti za jamii na kuhusu mayatima na wajane. Uislamu ukiwa kama dini ya dunia nzima unafaa kwa maeneo yote na nyakati zote kwa hiyo, haungepuuza shuruti na mambo ya lazima.

Katika jamii nyingi za wanadamu, wanawake ni wengi kuliko wanaume. Nchini Marekani kwa uchache, kuna wanawake milioni nane zaidi ya wanaume. Katika nchi kama vile

Guinea kuna wanawake 122 kwa kila wanaume 100. nchini Tanzania, Kuna wanaume 95.1 kwa kila wanawake 100.[55] Jamii ifanye nini kuhusu huu uwiano wa kijinsia usio na ulingano? Kuna utatuzi wa aina mbali mbali, baadhi wanaweza kupendekeza useja, wengine wangependelea kuwauwa watoto wachanga wakike (Jambo litokealo katika baadhi ya jamii ulimwenguni leo hii!) Wengine wangedhani kuwa tundu pekee ya kutokea kutoka katika tatizo hilo ni kuwa jamii isamehe aina zote za ngono: umalaya, ngono nje ya ndoa, kusagana, ushoga n.k. Kwa jamii nyingine, kwa mfano jamii nyingi za Kiafrika leo hii, dhana kuu inayoheshimika ni kuruhusu ndoa za mitala kama mila iliyokubaliwa na ni kitu kinachoheshimiwa na jamii. Nukta ambayo mara nyingi haifahamiki katika nchi za Kimagharibi ni kuwa wanawake katika jamii nyingine hawalitazami jambo la mitala kwa mtazamo wa dhulma ya kudhalilishwa. Kwa mfano mabibi harusi wadogo wadogo wengi, Wakristo, Waislamu au watu wengine, wanapendelea kuolewa na mwanamume aliyeoa na ambaye tayari huyo mwanamume mwenyewe amejitolea awe mume mwenye kubeba majukumu.

Wake wengi wa Kiafrika wanawataka waume zao waoe mke wa pili ili wasijihisi wapweke.[56] Uchunguzi uliowahusisha zaidi ya wanawake elfu 6, wenye umri wa kati ya miaka 15

[55] Ibid., pp. 92. 88-93.
[56] Ibid., pp. 92-97.

hadi 59, walio katika mji wa pili kwa ukubwa nchini Nigeria wameonyesha kuwa asilimia sitini 60% ya wanawake hao watafurahi kama waume zao wataoa wake wengine. Ni asilimia 23% tu walioonyesha kukerwa na wazo la ukewenza. Asilimia 76% ya wanawake waliofanyiwa uchunguzi nchini Kenya walionyesha kukubali mitala.

Uchunguzi uliofanywa vijijini Kenya, wanawake 25 katika kila 27 wanapendelea ukewenza kuliko kuwa mke mmoja tu. Wanawake hao wanahisi kuwa ukewenza ni furaha na unafaida kama wake wenza watashirikiana na kusaidiana.[57] Ukewenza katika jamii nyingi za Kiafrika ni msingi unaoheshimika kwa kiasi ambacho baadhi ya Makanisa ya Kiporestanti yamekuwa yakiruhusu mitala. Askofu wa Kanisa la Kianglikana nchini Kenya ametangaza kuwa, "*Ingawa kutokuwa na mitala huenda likawa ni jambo bora kwa kuelezea mapenzi kati ya mume na mke, Kanisa lazima lizingatie kuwa katika baadhi ya tamaduni mitala ni jambo linalokubaliwa na jamii na kuwa imani ya kuwa mitala ni kinyume na Ukristo si ya kufuatwa tena.*[58]

Baada ya uchunguzi yakinifu juu ya mitala ya Waafrika, Reverend David Gitari wa Kanisa la Kianglikana amehitimisha kuwa mitala ni bora kufanywa, na ndio Ukristo zaidi kuliko talaka na kuoa tena, ili kuwaonea huruma wake

[57] Philip L. Kilbride, Plural Marriage For Our Times (Westport, Conn.: Bergin & Garvey, 1994) pp. 108-109.
[58] The Weekly Review, Aug. 1, 1987.

walioachwa na watoto wao.[59] Mimi binafsi nafahamu baadhi ya wake wa Kiafrika waliosoma sana na ambao, ingawa wamewahi kuishi Ulaya Magharibi kwa miaka mingi, hawana pingamizi juu ya mitala. Mmoja wao, anayeishi Marekani, kwa dhati kabisa anamsihi mumewe aoe mke wa pili ili amsaidie kulea watoto.

Tatizo la ujinsia usio na uwiano limekuwa ni tatizo sugu nyakati za vita. Makabila ya Wahindi Wekundu, watu asilia wa Marekani walikuwa wanasumbuliwa kwa kiasi kikubwa na tatizo la ujinsia usio na uwiano baada ya kumalizika vita wakiwa wameshindwa. Wanawake katika makabila hayo, ambao kwa hakika walifurahia hali ya kijamii ya hali ya juu, walikubali mitala kuwa ndio kinga bora zaidi dhidi ya matendo ya mahusiano yasiyo na heshima. Walowezi wa Ulaya, bila ya kutoa tiba mbadala, walilaani mitala ya Wahindi na kudai kuwa ni watu wasiostaarabika.[60] Baada ya vita vya pili vya Dunia, kulikuwa na wanawake 7,300,000 zaidi ya wanaume nchini Ujerumani (milioni 3.3 miongoni mwao walikuwa wajane).

Kulikuwa na wanaume 100 wenye umri wa miaka 20 hadi 30 kwa kila wanawake 167 walio katika umri wa kuolewa.[61]

---

[59] Kilbride, op. cit., p. 126.
[60] John D`Emilio and Estelle B. Freedman, Intimate Matters: A history of Sexuality in America (New York: Harper & Row Publishers, 1988) p. 87.
[61] Ute Frevert, Women in German History: from Bourgeois Emancipation to Sexual Liberation (New York: Berg Pulishers, 1988) pp. 263-264.

Wengi wa wanawake hao wanahitaji mwanamume si wa kukaa naye tu lakini pia awe wa kuleta matumizi ya nyumbani katika nyakati za umasikini usio na kifani na hali ngumu. Majeshi ya muungano yaliyoshinda yaliwanyonya wanawake hao kwa sababu ya shida zao. Wasichana na wajane wengi walijihusisha katika mahusiano ya kiasherati na wanajeshi wa majeshi ya uvamizi. Wanajeshi wengi wa Kimarekani na Kiingereza walikuwa wakitoa sigara, chokoleti, na mikate kama malipo ya kustarehe na wanawake hao. Watoto walikuwa wanafurahia sana zawadi hizo zilizotolewa na wageni hao.

Mtoto wa kiume wa umri wa miaka 10 aliposikia zawadi hizo kwa watoto wengine, kwa moyo wake wote alitamani aje "Muingereza" kwa mama yake ili wasife njaa.[62]

Lazima tuulize dhamira zetu kuhusu nukta hii: Nini kinamtukuza zaidi mwanamke? Kukubali na kuheshimu mke wa pili kama ilivyo kwa mtazamo wa Wahindi wekundu au umalaya wa hakika usio bayana kama ulivyo kwa mtazamo wa watu wenye kustaarabika? Kwa maneno mengine, kipi ni chema zaidi kwa mwanamke, maagizo ya Quran au itikadi inayotegemea utamaduni wa Himaya ya Kirumi?

Ni jambo la kuvutia kujua kwamba katika mkutano wa kimataifa wa vijana uliofanyika Munich mwaka 1948 tatizo la ujinsia usio na uwiano nchini Ujerumani lilijadiliwa. Na

[62] Ibid., pp. 257-258.

ilipodhihirika kwa uwazi kuwa hakuna dawa iliyoafikiwa, baadhi ya washiriki walipendekeza mitala. Jibu la kwanza la washiriki wa mkutano huo lilikuwa ni mchanganyiko wa mshtuko na kero. Hata hivyo, baada ya uchunguzi wa kina juu ya pendekezo hilo, washiriki walikubaliana kuwa jambo hilo lilikuwa ndio utatuzi wa pekee. Kwa hiyo, mitala ilihitimishwa kuwa ni miongoni mwa mapendekezo ya mwisho ya mkutano huo.[63]

Ulimwengu leo hii unamiliki silaha nyingi za maangamizi kuliko ilivyokuwa hapo kabla na makanisa ya Ulaya hivi karibuni au baadaye, yatalazimika kukubali mitala kuwa ndio njia pekee. Baba Hillman ameufahamu kiakili sana hakika hiyo, *"Ni ukweli kwamba silaha za kuangamiza (nyukilia, vijidudu na kemikali…) zitaleta kutokuwa na uwiano wa kijinsia kwa hiyo, mitala itakuwa ni jambo la lazima ili kunusurika…. Kisha kinyume na utamaduni na sheria zilizotangulia, tabia ya kuchosha na heshima za kiutu zitaibua tukio la kuthaminiwa kwa mitala. Katika hali kama hiyo, wananchi na viongozi wa kanisa haraka haraka watatunda sababu nzito nzito na maandiko ya Biblia ili kuhalalisha itikadi mpya ya ndoa.*[64]

Leo hii, mitala inaendelea kuwa ni utatuzi wa kijitosheleza kwa baadhi ya matatizo ya kijamii katika jamii za kisasa.

[63] Sabiq., op. cit., p. 12.
[64] Hillman, op. cit., p. 12.

Masharti ya kijamii ambayo yanaonyeshwa na Quran yakishirikiana na ruhusa ya mitala ni jambo linaloonekana sana leo hii katika baadhi ya jamii za Kimagharibi, kuliko Afrika. Kwa mfano, nchini Marekani leo hii, kuna matatizo makali sana ya ujinsia katika jamii za watu weusi. Kijana mmoja katika kila vijana weusi wa kiume kumi anakufa kabla ya kufikia umri wa miaka 21. Kwa wale walio na umri wa miaka kati ya 20 na 35, mauaji ndiyo sabau kuu ya vifo vyao.[65]

Aidha, vijana weusi wengi hawajaajiriwa, wapo jela, au wanatumia dawa za kulevya.[66] Matokeo yake, mmoja kati ya wanawake weusi wanne, wenye umri wa miaka 40, hajaolewa, ukilinganisha na mwanamke mmoja katika kila wanawake kumi wa kizungu.[67]

Zaidi ya hayo, wanawake weusi wengi wanakuwa ni wazazi wasio na mume kabla ya umri wa miaka 20 na wanajikuta wanashida ya kutokuwa na mtu wa kuwatafutia ridhiki. Matokeo ya mwisho ya hali hiyo ya kuhuzunisha ni kuongezeka idadi ya wanawake weusi wenye uhusiano ujulikanao kwa jina la "kuchangia-bwana."[68]

---

[65] Nathan Hare and Julie Hare, ed., Crisis in Black Sexual Politics (San Francisco: Black Think Tank, 1989) p. 25.
[66] Ibid., p. 26.
[67] Kilbride, op. cit., p. 94.
[68] Ibid., p. 95.

Hiyo ni kwa kuwa, wengi wa wanawake hao weusi wasio na waume, wana bahati mbaya na wana uhusiano wa kiuasherati na wanaume waliooa. Wake nao mara nyingi wanakuwa hawatambui ukweli kwamba wanawake wengine wanashirikiana nao kwa waume zao. Baadhi ya waangalizi wa migogoro ya kuchangia bwana katika jamii ya Wamarekani Waafrika kwa uzito mkubwa wamependekeza mitala yenye mwafaka kuwa ndilo jibu la muda kwa tatizo la wanaume weusi hadi hapo mapinduzi kamilifu yatakapopatikana katika jamii ya Kimarekani.[69]

Kwa kukubali mitala wanakusudia mitala ambayo imeruhusiwa na jamii na ile ambayo wahusika wote wameikubali kama ni mbadala wa ada ya siri ya kuchangia bwana ambayo inawadhuru wote wawili mke na jamii yote kiujumla. Tatizo la kuchangia mwanamume katika jamii ya Wamarekani Waafrika lilikuwa ndio mada ya kujadiliwa na jopo katika Chuo Kikuu cha Temple Philadelphia mnamo Januari 27, 1993.[70] Baadhi ya wazungumzaji walipendekeza mitala kuwa ni moja ya utatuzi unaowezekana kwa mgogoro huo. Pia walipendekeza kuwa mitala isiharamishwe na sheria, hasa katika jamii zinazoruhusu umalaya na vimada. Maelezo ya mwanamke mmojawapo miongoni mwa waliohudhuria amesema kuwa Wamarekani Waafrika wanatakiwa wajifunze

[69] Ibid.
[70] Ibid., pp. 95-99.

kutoka Afrika ambako mitala inafanyika kwa kubembeleza, mapenzi na nderemo.

Philip Kilbride, mwana anthropolojia- (mtaalamu wa elimu ya asili na maendeleo ya mwili wa mwanadamu)- ya urithi wa Romani Katoliki, katika kitabu chake cha uchokozi, Ndoa ya Wengi kwa Wakati wetu, anapendekeza mitala kama ni ufumbuzi wa baadhi ya matatizo ya kijamii za Kimarekani huru. Amedai kuwa ndoa za wengi huenda zikahudumia mbadala unaowezekana, mbadala wa talaka katika hali nyingi ili kuondoa mmomonyoko wa talaka kwa watoto wengi. Ameonyesha kuwa talaka nyingi zinasababishwa na kutapakaa kwa ngono za nje ya ndoa katika jamii za Kimarekani. Kwa mujibu wa Kilbride, kumaliza ngono za nje ya ndoa kwa kuoa wake wengi, ni bora kwa watoto kuliko talaka, *"Watoto wataokolewa vizuri kama tutadumisha familia zisitengane na kuporomoka, limeonekana ni chaguo mojawapo*." Zaidi ya hayo, anapendekeza kuwa makundi mengine vile vile yatafaidika kutokana na ndoa za wengi kama vile: wanawake wakongwe ambao wanakabiliana na tatizo la ukosefu wa wanaume na Waamerika Waafrika ambao wanajihusisha na kuchangia mwanamume.[71]

Mwaka 1987, kura ya maoni iliyoendeshwa na gazeti la wanafunzi wa chuo kikuu cha California cha Barkeley iliwauliza wanafunzi kama wanakubali kuwa wanaume

[71] Ibid., p. 118.

waruhusiwe na sheria wawe na mke zaidi ya mmoja ili kutambua na kujibu upungufu wa wanaume waoao mjini California. Takriban wanafunzi wote waliopiga kura wamekubali wazo hilo. Mmoja wa wanafunzi wa kike alieleza kuwa ndoa za mitala zitatimiza hisia zake na mahitaji yake ya kimwili huku akijipatia uhuru mkubwa kuliko itakavyokuwa kwa ndoa za mmoja tu.[72] Kwa hakika, madai kama hayo pia yanatumiwa na baadhi ya wanawake wachache wenye msimamo mkali ambao bado wanaendelea kutekeleza mitala nchini Marekani wao wanaamini kuwa ukewenza ni njia bora kwa mwanamke ili apate mambo mawili; matunzo na watoto kwa kusaidiana hao wake wenyewe kwa wenyewe kuwalea watoto.[73]

Lazima tuongeze kuwa mitala ya Uislamu ni jambo la makubaliano ya pande mbili. Hakuna mtu wa kumlazimisha mwanamke aolewe na mume aliyeoa. Aidha, mke ana haki kushurutisha kuwa mumewe asioe mwanamke mwingine kama mke wa pili.[74] Biblia, kwa upande mwingine na wakati mwingine inakimbilia ndoa za mitala za lazima. Mjane asiye na mtoto lazima aolewe na ndugu wa mumewe, hata kama tayari ameshaoa (tazama sehemu ya "*Matatizo ya Wajane*"), bila kujali radhi zake. (Mwanzo 38:8-10).

---

[72] Lang, op. cit., p. 172.
[73] Kilbride, op. cit., pp. 72-73.
[74] Sabiq, op. cit., pp. 187-188.

Ifahamike kuwa katika jamii nyingi za leo hii suala la kutekeleza mitala ni chache mno kwa kuwa mwanya kati ya idadi ya jinsia mbili ya kike na ya kiume si mkubwa. Mtu, kwa kujiamini, anaweza kusema kuwa kiwango cha ndoa za mitala katika ulimwengu wa Kiislamu ni kidogo sana kulinganisha na kiwango cha ngono za nje ya ndoa katika nchi za Kimagharibi. Kwa maneno mengine, wanaume katika ulimwengu wa Kiislamu leo hii ni wapenda mke mmoja sana kuliko wanaume katika nchi za Kimagharibi.

Billy Graham, mwinjilisti maarufu wa Kikristo ameutambua ukweli huo: "*Wakristo hawawezi kuafiki suala la mitala. Kama sasa hivi Wakristo hawawezi kufanya hivyo, huko ni kujivunja wenyewe. Uislamu umeruhusu mitala kama ni utatuzi wa matatizo ya kijamii na umeruhusu kiwango maalumu cha uhuru wa kimaumbile ya kibinadamu lakini hayo yote yakiwa katika mzingo wa sheria kali zilizotambulishwa. Nchi za Kikristo zinaonyesha maonyesho makubwa ya ndoa za mke mmoja, lakini kwa hakika zinatekeleza mitala. Hakuna mtu asiye na mwanamke zaidi ya mkewe, kuna vimada vinavyowekwa katika jamii za Kimagharibi. Kwa hiyo, Uislamu ni dini ya kuheshimika yenye wema wa kimsingi, na umemruhusu Mwislamu aoe mke wa pili kama atalazimika, lakini pia umeharamisha vikali*

*mno aina zote za ndoa za siri na uzinzi unaohusika ili kulinda uaminifu wa kimaadili wa jamii.*"[75]

Ni jambo la kuzingatia kuwa, katika nchi zisizo za Kiislamu na za Kiislamu ulimwenguni, leo hii, kuna mitala ya kinyume cha sheria. Kujitwalia mke wa pili hata kwa radhi za mke wa kwanza, ni uvunjaji wa sheria. Kwa upande mwingine, kumdanganya mke, bila kujua au kutoa radhi zake, ni jambo linalokubalika kisheria kabisa kabisa! Sasa ni nini hekima ya kisheria nyuma ya mgongano kama huo? Je, sheria imetungwa ili kuwazawadia wadanganyifu na kuwaadhibu wema? Jambo hilo ni moja ya fumbo lisilofikiwa utatuzi la ulimwengu wetu wa kisasa '*uliostaarabika'*.

[75] Abdul Rahman Doi, Woman in Shari`ah (London: Ta-Ha publishers, 1994) p. 76.

# SEHEMU 15

# HIJABU

Mwisho, acha tuangazie kile kinachohesabika katika nchi za Kimagharibi kuwa ni alama kuu ya kukandamizwa wanawake na kufanywa watumwa, kitu chenyewe ni hijabu au kufunika kichwa. Je, hivi ni kweli kwamba hakuna kitu kama hijabu katika itikadi ya Kiyahudi-Kikristo? Acha tunukuu moja kwa moja. Kwa mujibu wa Rabbi Dr. Menachen M. Brayer (Profesa wa Maandiko ya Biblia wa Chuo Kikuu cha Yeshiva) katika kitabu chake, Mwanamke wa Kiyahudi katika mafundisho ya Kirabbiniki, ilikuwa ni desturi ya wanawake wa Kiyahudi kutoka nje kwenye watu wengi wakiwa na vifuniko vya vichwa ambavyo, wakati mwingine, vilikuwa vinafunika uso wote na kuacha jicho moja tu.[76] Alinukuu baadhi ya maneno ya wanazuoni wa kale wa Kiyahudi ambao ni mashuhuri, *"Si katika mabinti wa Kiyahudi watembeao nje bila ya kufunika kichwa"* na *"Laana iwe kwa mtu anayeruhusu nywele za mkewe zionekane…. mwanamke anayefunua nywele zake kwa kujipamba anasababisha umasikini."* Sheria ya Kirabbiniki inakataza kukariri maneno matakatifu au sala mbele ya

[76] Menachem M. Brayer, The Jewish Woman in Rabbinic Literature: A Psychosocial Perspective (Hoboken, N.J: Ktav Publishing House, 1986) p. 239.

mwanamke aliyeolewa na aliye kichwa wazi kwa kuwa kutofunikwa kwa nywele za mwanmke kunachukuliwa kuwa ni "*kukaa uchi*." [77]

Dr. Brayer vile vile ametaja kuwa "*katika zama za Tunnaitiki,*" *mwanamke wa Kiyahudi anayeshindwa kufunika kichwa chake alihesabiwa kuwa anafedhehesha utu wake. Na pindi kichwa chake kinapofunuka atalipishwa faini ya Zumzim mia nne kwa sababu ya dhambi hiyo*." Dr. Brayer vile vile amefafanua kuwa hijabu ya mwanamke wa Kiyahudi sio siku zote ilikuwa inazingatiwa kuwa ni alama ya wema. Wakati mwingine, hijabu ilikuwa inaonyesha alama ya upambanuzi na anasa kuliko wema. Hijabu inatoa mfano wa ufahari na ubora zaidi wa mwanamke mwema. Vile vile inawakilisha nafasi ya mwanmke isiyofikika ikiwa ni mali takatifu ya mumewe.[78]

Hijabu ni alama ya heshima binafsi ya mwanamke na nafasi ya kijamii. Wanawake wa daraja la chini mara nyingi walivaa hijabu ili waonekane kuwa ni wa hali ya juu. Ukweli wa kuwa hijabu ilikuwa ni alama ya uungwana ndiyo iliyokuwa sababu iliyowafanya malaya kuzuiwa kufunika nywele zao katika jamii ya kale ya Kiyahudi. Hata hivyo, malaya wakati

[77] Ibid., pp. 316-317. Also see Swidler, op., cit., pp. 121 – 123.
[78] Ibid., p. 139.

mwingine walikuwa wanavaa vitambaa maalumu vya kichwani ili waonekane kuwa ni wenye heshima.[79]

Wanawake wa Kiyahudi katika nchi za Ulaya waliendelea kuvaa hijabu hadi karne ya kumi na tisa wakati maisha yao yalipochanganyika sana na utamaduni wa usiofuata dini (kisekyula) uliowazunguka. Starehe za nje za maisha ya Kiulaya katika karne ya kumi na tisa iliwalazimisha wengi wao watoke nje vichwa wazi. Baadhi ya wanawake wa Kiyahudin walionelea ni jambo la kufaa zaidi kubadilisha utamaduni wao wa hijabu na nywele bandia zikiwa ni kama mtindo mwingine wa kufunika kichwa. Leo hii, wanawake wa Kiyahudi halisi wengi hawafuniki nywele zao ila sinagogini.[80] Baadhi yao, kama vile wa madhehebu ya Hasidiki, wanaendelea kutumia nywele bandia.[81]

Je, mafundisho ya Kikristo yana nini? Ni jambo maarufu sana kuwa watawa wa Kikatoliki wamefunika vichwa vyao kwa mimia ya miaka, lakini hilo si la mwisho. Mt. Paulo katika Agano Jipya ameweka maelezo ya kuvutia sana kuhusiana na hijabu:

"*Lakini nataka mjuwe ya kuwa kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, na kichwa cha mwanamke ni mwanamume, na*

[79] Susan W. Schneider, Jewish and Female (New York: Simon & Schuster, 1984) p. 237.
[80] Ibid., pp. 238-239.
[81] Alexandra Wright, "Judaism", in Holm and Bowker, ed., op. cit., pp. 128-129.

*kichwa cha Kristo ni Mungu. Kila mwanamume, asalipo, au anapohutubu, naye amefunikwa kichwa, yuaabisha kichwa chake. Bali kila mwanamke asalipo, au anapohutubu, bila kufunika kichwa, yuaabisha kichwa chake; kwa maana ni sawasawa na yule aliyenyolewa. Maana mwanamke asipofunikwa na akatwe nywele. Au ikiwa ni aibu mwanamke kukatwa nywele zake au kunyolewa na afunikwe. Kwa maana kweli haimpasi mwanamume kufunikwa kichwa, kwa sababu yeye ni mfano na utukufu wa Mungu. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume. Maana mwanamume hakutoka katika mwanamke, bali mwanamke katika mwanamume. Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume. Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani, kwa ajili ya malaika*." (1 Wakorintho 11:3-10)

Mantiki ya Mt. Paulo kuhusu suala la hijabu za wanawake ni kuwa hijabu inawakilisha alama ya mamalaka ya mwanamume, ambaye ni sura na utukufu wa Mungu, juu ya mwanamke ambaye aliumbwa kutoka kwa mwanamume na kwa ajili ya mwanamume. Mt. Tertullian katika makala zake mashuhuri "Juu ya Hijabu Ya Mabikira'' aliandika, "*Wasichana, vaeni hijabu zenu mkiwa nje mitaani, hivyo hivyo mzivae makanisani, mzivae mnapokuwa na wageni, kisha zivaeni mkiwa na kaka zenu*…." Miongoni mwa sheria za kikanuni za kanisa Katoliki leo hii, kuna sheria ambayo

inawaagiza wanawake wafunike vichwa vyao makanisani.[82] Baadhi ya madhehebu ya Kikristo, kama vile Waamish na Wameminites wanaendelea kuwavalisha hijabu wanawake zao hadi siku hizi. Lengo la hijabu, kama lilivyotolewa na viongozi wao wa Kanisani, ni kuwa "*Kufunikwa kichwa ni alama ya kutii kwa mwanamke kumtii mwanamume na Mungu.*" Ambayo ni mantiki ile ile iliyotolewa na Mt. Paulo katika Agano Jipya.[83]

Kutokana na ushahidi wote huo uliotangulia, ni wazi kuwa Uislamu haujazua hijabu. Hata hivyo, Uislamu umeithibitisha hiyo hijabu. Quran inawataka waumini waume kwa wake wainamishe macho yao na walinde heshima zao na kisha inawataka waumini wa kike wajitande hijabu na kufunika shingo na kifua:

"*Waambie wanaume wainamishe macho Yao (wasitazame yaliyokatazwa), na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao; bila shaka Mwenyezi Mungu anazo habari za (yote) wanayoyafanya. Na waambie wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasidhihirishe viungo vyao ispokuwa vinavyodhihirika (nao ni uso na vitanga vya mikono - na wengine wanasema na nyayo). Na waangushe*

---

[82] Clara M. Henning, "Cannon Law and the Battle of the Sexes" in Rosemary R. Ruether, ed., Religion and Sexism: Images of Weoman in the Jewish and Christian Traditions (New York: Simon and Schuster, 1974) p. 272.
[83] Donald B Kraybill, The riddle of the Amish Culture (Baltimore: Johns Hopkins University Press, 1989) p. 56.

*shungi zao mpaka vifuani mwao, na wasionyeshe mapambo yao ila kwa waume zao, au baba zao…”* (Quran 24:30-31)

Quran ipo wazi kabisa, kuwa hijabu ni asili ya wema na kujihifadhi, lakini kwa nini iwe kujihifadhi ni muhimu? Quran bado inaendelea kuwa wazi:

“*Ewe Mtume! Waambie wake zako, na binti zako, na wanawake wa Kiislamu (wangine - waambie) wajiteremshie uzuri nguo zao. Kufanya hivyo kutapelekea upesi wajulikane (kuwa ni watu wa hishima ili) wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.”* (Quran 33:59)

Hii ndiyo hoja kamili, heshima imeelezwa kuwa ni kinga kwa wanawake wasiudhiwe au kugeuzwa ni kitu rahisi rahisi, heshima ni kinga. Kwa hiyo, lengo pekee la hijabu katika Uislamu ni kinga. Hijabu ya Kiislamu, ni kinyume na ya mafundisho ya Kikristo, si alama ya mamlaka ya mwanamume kwa mwanamke wala si alama ya utiifu wa wanawake kwa wanaume. Hijabu ya Kiislamu ni kinyume na ya mafundisho ya Kiyahudi, si alama ya anasa na kujitenga kwa baadhi ya wanawake wa tabaka la juu walioolewa. Hijabu ya Kiislamu, ni alama ya heshima tu ikiwa na lengo la kuwakinga wanawake, wanawake wote. Hekima ya Kiislamu ni kuwa siku zote ni bora kusalimika kuliko kupewa pole. Kwa hakika, Quran inazingatia sana suala la kulinda miili ya wanawake na sifa zao kiasi ambacho mwanamume

anayethubutu kumsingizia mwanake kuwa ni mzinifu ataadhibiwa vikali:

"*Na wale wanaowasingizia wanawake watahirifu (kuwa wamezini), kisha hawaleti mashahidi wanne, basi wapigeni mijeledi, (bakora) thamanini, na msiwakubalie ushahidi wao tena, na hao ndio mafasiki*." (Quran 24:4)

Linganisha mtazamo huu mkali wa Quran na adhabu ya kustarehesha kabisa kwa kosa la kubaka iliyo katika Biblia: "*Mtu mume akimwona kijana aliye mwanamwali ambaye hajaposwa akamshika na kulala naye, wakaonekana; yule mtu mume aliyelala naye na ampe baba yake yule kijana shekeli hamsini za fedha, kisha na awe mkewe kwa, kuwa amemtweza; hana ruhusa ya kumwacha siku zake zote*." (Kumbukumbu 22:28-39)

Hapa mtu lazima aulize swali lepesi, ni nani hasa aliyeadhibiwa? Mtu aliyelipishwa faini tu kwa kubaka, au yule msichana aliyelazimishwa kuolewa na mtu aliyembaka na aishi naye hadi afe? Swali lingine ambalo pia, linatakiwa liulizwe ni hili: Ni jambo lipi linalowalinda sana wanawake, je, ni mtazamo mkali wa Kiquran au mtazamo wa kustarehesha wa Kibiblia?

Baadhi ya watu na hasa hasa wa Ulaya Magharibi, wanakusudia kuyadhihaki madai yote yanayodai kujiheshimu kuwa ni kinga. Madai yao ni kuwa; kinga bora zaidi ni kueneza elimu, tabia za kistarabu, na kujizuia. Sisi tunasema:

Ni jambo zuri lakini halitoshi. Kama 'ustaarabu' ni kinga ya kutosha, kwa nini wanawake wa nchi za Amerika ya Kaskazini hawathubutu kutembea peke yao katika mitaa yenye kiza – au katika eneo kubwa la wazi? Kama Elimu ni jibu, kwa nini chuo kikuu kinachoheshimika sana cha Queen kina 'huduma ya kurudisha nyumbani' na hasa hasa wanafunzi wa kike katika eneo la chuo?

Kama kujizuia ni jibu, kwa nini mashitaka ya unyanyasaji kijinsia makazini yanaripotiwa katika vyombo vya habari kila siku? Mfano wa mashitaka ya unyanyasaji wa kijinsia, katika kipindi cha miaka michache iliyopita, inakusanya: Maofisa wa jeshi la wanamaji, Mameneja, Maprofesa wa vyuo vikuu, Maseneta, Wakuu wa mahakama, na Raisi wa Marekani!

Sikuweza kuamini macho yangu, niliposoma maelezo yafuatayo, yaliyoandikwa katika waraka uliotolewa na Mkuu wa ofisi za wanawake wa chuo kikuu cha Queen:

Nchini Canada, kila dakika 6 mwanamke mmoja anashambuliwa kijinsia,

Mwanamke mmoja katika kila wanawake watatu nchini Canada atashambuliwa kijinsia muda wowote ule maishani mwake.

Mwanamke mmoja katika kila wanawake wanne yupo hatarini kubakwa au kujaribiwa kubakwa maishani mwake,

Mwanamke mmoja katika kila wanawake wanane atashambuliwa kijinsia wakati akiwa anahudhuria chuoni, na

Uchunguzi umegundua kuwa aslimia sitini 60% ya wavulana wa vyuo vikuu vya Canada wamesema watatenda shambulio la kijinsia ikiwa wataona kuwa hawatakamatwa.

Kuna makosa makubwa mno katika jamii tunamoishi. Mabadiliko ya kina katika mtindo wa maisha ya kijamii lazima yafanyike. Utamaduni wa kujiheshimu unahitajika ile mbaya, kujiheshimu kimavazi, maongezi, na tabia za wanaume na wanawake. Vinginevyo mikwaruzano mikali itaongezeka na kuwa mibaya zaidi siku baada ya siku, na kwa bahati mbaya. Wanawake peke yao ndio watakaoathirika sana. Watalipia thamani ya hayo. Kwa hakika sote tunaumia lakini kama Bw. K. Gibran alivyosema, "…mtu anaepata vipigo si sawa na yule anayevihesabu."[84] Kwa hiyo, jamii kama ya Ufaransa ambayo inawafukuza shule wasichana kwa sababu ya nguo zao za kujiheshimu, nchi hiyo ipo mwishoni, na inajibomoa yenyewe kirahisi.

Ni moja ya kejeli kubwa katika ulimwengu wetu wa leo kuwa kifuniko cha kichwa kinachovaliwa kwa lengo la kuonyesha "utakatifu" na mamlaka ya mwanamume, kinapovaliwa na watawa wa Kikakotoliki, hakina tatizo. Na kifuniko hicho kinakuwa kinaonyesha alama ya kukandamizwa wanawake

[84] Khalil Gibran, Thoughts and Meditations (New York: Bantam Books, 1960) p. 28.

pale kinapovaliwa kwa lengo la kujihifadhi na wanawake wa Kiislamu.

# SEHEMU 16

# HITIMISHO

Swali la pekee ambalo wasiokuwa Waislamu, ambao wameshasoma maelezo yaliyotangulia ya uchunguzi huu, ni: Je, wanawake wa Kiislamu ulimwenguni leo hii wanapata huduma hizo nzuri nzuri zilizotajwa humu? Jibu, kwa bahati mbaya ni: Hapana, kwa kuwa, swali hili lisiloepukika katika majadiliano yoyote yanayowahusu wanawake katika Uislamu, lazima tuchanganue jibu hilo ili tumpatie msomaji picha kamili.

Kwanza, ni lazima iwekwe wazi kuwa, tofauti kubwa kati ya jamii za Waislamu zinafanya kuwajumuisha kuwa ndilo jambo lilorahisi sana. Kuna vivuli vipana mno vya kimtazamo juu ya wanawake katika ulimwengu wa Kiislamu leo hii. Mitazamo hiyo inatofautiana toka jamii moja hadi nyingine na ndani ya jamii moja yenyewe kwa yenyewe. Bila kujali, mitazamo ya kiujumla iliyo maalumu na unayotambulika. Takriban jamii zote za Kiislamu kwa daraja moja au nyingine, zimekengeuka na kuacha ukamilifu wa Kiislamu unaoheshimu nafasi ya wanawake. Kukengeuka huko, kwa sehemu kubwa, kumekuwa katika mwelekeo mmoja kati ya miwili inayopingana. Mwelekeo wa kwanza ni wa kung`ang`ania sana kwa imani kali ya tamaduni za

Kimashariki (Kiarabu). Huku mtazmo wa pili ukiwa ni wa Kiliberali (uhuru) sana na ni wa tamaduni za Kimagharibi (Kizungu).

Jamii iliyokengeuka na kufuata mwelekeo wa kwanza inawatendea wanawake kulingana na mila na tamaduni zilizorithiwa kutoka kwa mababu zao. Mila hizo mara nyingi zinawanyima wanawake haki nyingi walizopewa na Uislamu. Aidha, wanawake wanatendewa kwa vigezo tofauti kabisa na vile wanavyotendewa wanaume. Ubaguzi huo unasambaa katika maisha ya kila mwanamke: mwanamke anapata kufurahiwa kidogo tu wakati anapozaliwa kuliko mwanamume; hapelekwi shule; ananyimwa fungu katika mirathi ya familia yake; yupo chini ya upelelezi unaoendelea ili asiende kinyume huku ikiwa kwenda kinyume kwa kaka yake kunavumiliwa; anaweza kuuliwa kwa kutenda kile ambacho ndugu zake wa kiume siku zote wanajisifu kwa kukitenda; hana kauli ila mara chache tena katika mambo ya kifamilia au mapendekezo ya kijamii; yeye anaweza kuwa hana madaraka kamili kwa mali yake na mahari ya ndoa yake; mwisho akiwa ni mama, yeye mwenyewe anaweza kupendelea kuzaa watoto wa kiume ili apate nafasi bora katika jamii yake.

Kwa upande mwingine, kuna jamii za Kiislamu (au baadhi ya matabaka maalumu ndani ya baadhi ya jamii) ambao wamesombwa na tamaduni na njia za maisha za Kimagharibi. Jamii hizi mara nyingi zinaiga bila kufikiria, chochote wakipokeacho kutoka Magharibi na mara nyingi wanaishia

kuathirika na kuambulia matunda yaliyooza ya Ustaarabu wa Kimagharibi. Katika jamii hizi, Usasa wa aina yake, wa ufahari wa hali ya juu wa maisha ya mwanamke ni kuzidisha uzuri wa mwili wake. Kwa hiyo, ameshikwa na umbo la mwili wake, ukubwa, na uzito. Mwanamke anakusudia kuujali sana mwili wake kuliko akili zake na zaidi ni kuhusu haiba yake kuliko akili yake. Uwezo wake wa kiuzuri, kuvutia, na wa kuamsha vichocheo ni vitu vya thamani sana katika jamii hiyo kuliko mafanikio yake kielimu, ushughulikiaji wa kiakili, na kazi za kijamii. Mtu hawezi kukuta nakala ya Quran katika pochi yake kwa kuwa imejaa vipodozi ambavyo anakuwa navyo popote aendapo. Moyo wake hauna nafasi ya kushughulikia mambo ya kijamii kwa mvuto wake. Kwa hiyo, mwanamke huyo atatumia maisha yake akipambana na mambo mengi ili ajithibitishie uwanamke wake kuliko kutekeleza utu wake.

Kwa nini jamii za Kiislamu zinakengeuka na kuuacha ukamilifu wa Kiislamu? Hakuna jibu lepesi. Maelezo yanayojipenyeza juu ya sababu kwa nini Waislamu hawashikamani na muongozo wa Quran wa kuwaheshimu wanawake maelezo ambayo yatakuwa ni kinyume na uwezo wa uchunguzi huu. Ni lazima iwekwe wazi, hata hivyo, kuwa jamii za Kiislamu zimekengeuka kutoka katika maadili ya Uislamu unahusisha mitazamo mingi sana ya maisha, tena kwa upeo mkubwa. Kuna mwanya mpana kati ya kile wanachotegemewa kukiamini na kile wakifanyacho kwa hakika. Mwanya huu si tukio la hivi karibuni.

Mwanya huo umekuwepo kwa karne nyingi na unaendelea kupanuka siku baada ya siku. Mwanya huo unaopanuka sana una matokeo ya kuangamiza wigo wa ulimwengu wa Kiislamu, tena katika takriban mitazamo yote ya kimaisha: udhalimu wa kisiasa na maangamizi, uchumi kubaki nyuma, dhulma ya kijamii, kufilisika kisayansi, kudumaa kiakili, n.k, Nafasi ya mwanamke katika jamii za wasiokuwa Waislamu ulimwenguni leo hii ni dalili tu ya maradhi makubwa. Mapinduzi yoyote ya mkondo wa nafasi ya wanawake wa Kiislamu hayatarajiwi kukamilishwa kama hayajaambatana na mabadiliko kamili ya maisha jumla ya jamii za Waislamu. Ulimwengu wa Kiislamu unahitaji mwamko ambao utaupeleka karibu na ukamilifu wa Kiislamu na sio kuupeleka mbali mno. Ili kuhitimisha, wazo la kuwa nafasi mbaya ya wanawake wa Kiislamu leo hii ni kwa sababu ya kutofahamika (kupotoshwa) kabisa kabisa kwa Uislamu. Kwa ujumla matatizo yao ni kwa ajili ya kushambuliwa sana, wamefikia kilele kirefu cha upweke na jambo hilo.

Pia, ni lazima kutiliwe mkazo tena, kuwa lengo la utafiti linganishi huu si, kukashifu Uyahudi wala Ukristo, kwa namna yeyote ile.

Nafasi ya mwanamke katika itikadi ya Uyahudi-Ukristo inaweza kuonekana ni ya kushtua katika vigezo vya wakati wetu huu wa mwishoni mwa karne ya ishirini. Bila kujali, ni lazima iangaliwe kwa maandishi kamilifu ya kuhistoria. Kwa ibara nyingine, makadirio yoyote ya uadilifu juu ya nafasi ya wanawake katika itikadi ya Uyahudi-Ukristo ni lazima yatie

maanani matokeo ya kihistoria ambayo kwayo mafundisho hayo ndio yameanzia. Kutakuwa hakuna shaka yoyote kuwa mitazamo ya Marabbi na Mapadri wa makanisa ya kumtazama mwanamke yaliathiriwa na mitazamo mingi ya kuwaona wanawake katika jamii zao. Biblia yenyewe iliandikwa na waandishi tofauti tofauti na nyakati tofauti tofauti. Waandishi hao hawakuwa ni wenye kutopenyeka na kuheshimu njia za maisha za watu waliowazunguka. Kwa mfano, sheria ya uzinzi ya Agano la Kale inachuki sana dhidi ya wanawake kiasi ambacho inakataa maelezo ya kimantiki ya wanafalsafa.

Hata hivyo, kama tutazingatia ukweli kwamba makabila ya kwanza ya Kiyahudi yamejawa na hali moja ya kijenetiki na juhudi za upeo wa juu za kujitambulisha wao wenyewe binafsi na kujitenga na makabila yaliyowazunguka na kwa hiyo ngono ya uzinifu kwa mwanamke aliyeolewa kwa mataifa inaweza kutishia tamaa ya kutunza mila hiyo, tunatakiwa tufahamu, lakini si lazima kuionea huruma hoja ya upendeleo huu. Pia, makemeo ya Mapadri wa makanisa dhidi ya wanawake hayatokuwa na uadilifu kutokana na muktadha wa maelezo ya kuwachukia wanawake ya utamaduni wa Kigiriki-Kirumi ambao walikuwa wakiishi katika tamaduni hizo. Utakuwa si uadilifu kutothamini urithi wa Uyahudi-Ukristo bila ya kutoa muktadha wa maelezo husika.

Kwa hakika, ufahamu wa muktadha wa maelezo ya historia ya Uyahudi-Ukristo pia ni muhimu sana katika kufahamu

umuhimu wa mchango wa Uislamu katika historia ulimwenguni na ustaarabu wa wanadamu. Itikadi ya Kiyahudi-Kikristo zimeathiriwa na kuundwa na mazingira, hali na tamaduni zilipokuwapo katika tamaduni hizo. Hadi kufikia karne ya saba C.E., athari hizo zilipotosha sura asilia ya ujumbe mtakatifu uliofunuliwa kwa Musa na Yesu bila ya kutambua. Hali duni ya wanawake katika ulimwengu wa Kiyahudi-Kikristo katika karne ya saba ni moja ya hoja tu. Kwa hiyo, kulikuwa na haja kubwa ya ujumbe mtakatifu mpya ambao utaongoza wanadamu warejee katika njia iliyonyooka. Quran imefafanua kazi ya mjumbe mpya ni kuwaweka huru Wayahudi na Wakristo kutokana na mizigo mizito ambayo walikuwa wanaibeba: "*Ambao wanamfuata Mtume, Nabii aliye Ummy (asiyejua kusoma wala kuandika, na juu ya hivi atafundisha mafundisho hayo ya ajabu ya Uislamu), ambaye wanamuona ameandikwa kwao katika Taurati na Injili ambaye anawaamrisha mema na anawakataza yaliyo mabaya, na kuwahalalishia vizuri na kuwaharamishia vibaya, na kuwaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao (yaani sharia ngumu za zamani na mila za kikafiri). Basi wale waliomuamini yeye na kumuhishimu na kumsaidia na kuifuata Nuru iliyoteremshwa pamoja naye (yaani Quran) hao ndio wenye kufaulu.*" (Quran 7:157)

Kwa hiyo, Uislamu usitazamwe kuwa ni mpinzani wa itikadi ya Kiyahudi au Kikristo. Inatakiwa uzingatiwe kuwa ni kilele cha ukamilisho, na utimilifu wa ujumbe mtukufu ambao ulifunuliwa hapo kabla.

Mwisho wa uchunguzi huu, ningependa nitoe ushauri ufuatao kwa jamii ya Waislamu ulimwenguni. Wanawake wa Kiislamu wengi wamekuwa wakipinga haki zao za msingi za Kiislamu kwa muda mrefu. Makosa yaliyopita lazima yasahihishwe. Kufanya hivyo si kusaidia, huo ni wajibu usio na budi kwa kila Mwislamu. Jamii ya ulimwengu mzima lazima washughulikie mapatano ya haki za wanawake wa Kiislamu kwa misingi ya mafundisho ya Quran na Mtume wa Kiislamu. Mapatano hayo lazima yatawapa wanawake wa Kiislamu haki zote zilizotolewa kwao na Muumba. Kisha, mambo yote ya lazima, lazima yaendelezwe ili kuhakikisha utekelezaji mkamilifu wa mkataba huo. Mkataba huu unasubiriwa kwa muda mrefu, lakini ni bora kuchelewa kuliko kukosa kabisa. Ikiwa wa ulimwengu mzima hawatatoa dhamana ya kukamilisha haki zote za Kiislamu za mama zao, wake, dada, na mabinti zao, ni nani mwingine atakayefanya hivyo?

Kwa kuongezea, lazima tuwe na ushujaa wa kukabiliana na mambo yetu yaliyopita, na kuaacha papo hapo mila na tamaduni za wahenga wetu pale walipovunja sheria ya maadili ya Kiislamu. Je, Uislamu haukosoi vikali mila za wapagani wa Kiarabu za kufuata tamaduni za wazee wao kiupofu? Kwa upande mwingine, lazima tuendeleze mtazamo wa ukosoaji dhidi ya kila tunachopokea kutoka Magharibi au kutoka tamaduni nyingine zozote zile. Kuathiriana na kujifunza kutoka katika tamaduni za watu wengine ni jambo la thamani sana. Quran, kwa ufupi na uwazi, inazingatia kuathiriana huko kuwa ni moja ya malengo ya kuumbwa

kwetu. "*Enyi watu! Kwa hakika Tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja; Adamu) na (yule yule) mwanamke (mmoja; Hawwa). Na Tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane (tu basi; siyo mkejeliane)*.... (Quran 49:13). Kitu hicho kinaendelea lakini hakisemwi, hata hivyo, kuwaiga kibubusa watu wengine, kwa hakika ni alama ya kutojithamini.

Na kwa wasomaji wasiokuwa Waislamu, wawe Wayahudi, Wakristo au wowote wale, haya maneno ya mwisho ni wakfu. Ni jambo la kutatanisha kwa nini dini ambayo imefanya mapinduzi ya kumkomboa mwanamke imetengwa na kupakwa matope kuwa ni ya kukandamiza sana wanawake. Ufahamu huu juu ya Uislamu ni moja ya mauzauza yalioenea sana duniani leo hii. Mauzauza hayo yamekuwa yanaendelezwa na mlolongo usio na mwisho wa vitabu vya kusisimua, makala, taswira ya vyombo vya habari, na sinema za Hallwood. Matokeo yasioepukika ya mlolongo huu wa taswira ya kupotosha umekuwa ni kutofahamika kabisa kabisa na hofu juu ya kila kitu kinachofungamana na Uislamu. Taswira hii ya kuuona vibaya Uislamu katika vyombo vya habari ulimwenguni lazima ikome kama tunataka kuishi katika dunia huru iliyoepukana na mielekeo yote ya kibaguzi, madhara, na kupotosha. Wasiokuwa Waislamu wanatakiwa watambue kuwa kuna mwanya mpana kati ya imani ya Kiislamu na matendo ya Waislamu na ukweli mwepesi kuwa matendo ya si lazima yawe yanawakilisha Uislamu. Ili kutoa jina kwa nafasi ya mwanamke katika ulimwengu wa Kiislamu leo hii kuwa ni ya "*Kiislamu*" ni jambo lililombali sana na ukweli, sawa na

kuita nafasi ya mwanamke katika nchi za kimagharibi leo hii kuwa ni ya "*Kiyahudi-Kikristo*". Kwa ufahamu huu, Waislamu na wasio Waislamu lazima waanze hatua ya kuwasiliana na kuzungumza ili kuondosha upotoshaji, wasiwasi na hofu. Mustakabali wenye amani kwa familia ya kibinadamu unalazimisha kuwepo mazungumzo hayo.
Uislamu lazima utazamwe kama dini iliyoithibitisha sana nafasi ya wanawake na umewapa haki nyingi ambazo dunia ya kisasa umezitambua katika karne hii. Uislamu bado una mengi ya kuwapa wanawake wa kisasa: utu, heshima, na ulinzi katika kila nyanja na kila hatua ya maisha yake toka kuzaliwa hadi kifo, kwa kuongezea ili kutambulisha, kuwa na uwiano, na kima cha mahitajio yake yote ya kiroho, kifikra, kimwili na kimawazo. Si ajabu wengi wa wale wanaochagua kuwa wawe Waislamu katika nchi kama vile Uingereza ni wanawake. Nchini Marekani wanawake wanaobadili dini na kuwa Waislamu ni wengi zaidi kuliko wanaume kwa kiwango cha 4 kwa 1.[85]

Uislamu una mengi ya kuupa ulimwengu wetu ambao unahitaji sana mwongozo wa kimaadili uongozi. Balozi Herman Eilts, akitoa ushahidi mbele ya tume ya uhusiano wa mamabo ya nje katika baraza la wawakilishi-Congress la Marekani Juni 24, 1985, amesema, "*Idadi ya jamii ya Kiislamu ulimwenguni leo hii inakaribia bilioni moja. Na hiyo ni idadi ya kushtusha. Lakini kinachonishangaza zaidi ni*

[85] The Times, Nov. 18, 1993.

*kuwa leo hii Uislamu unakuwa haraka sana kuliko dini nyingine zenye kuamini Mungu mmoja. Jambo hili lazima tulizingatie. Kuna kitu cha haki katika Uislamu. Uislamu unawavutia watu wema wengi.*" Ndio, kuna haki katika Uislamu na huu ndio wakati wa kujua hivyo. Natarajia kuwa uchunguzi huu ni hatua mojawapo ya mwelekeo huo.

**Kimefasiriwa na**

**Bw. Omari Juma Mangilile,** Mwanafunzi katika Kitivo cha malezi na ualimu kiwango cha shahada ya uzamili chuo kikuu cha Cairo,

Na ni Mwanachama wa Tanzania Students Union (TSU)

E_mail:mangilile@yahoo.com

Cairo. (A.R.E).

*Kimepitiwa na,*

*Bw. Mohammed Sultani Ngunde*